# UTOHOZI WA WA MANENO-MKOPO KATIKA LUGHA YA KIJALUO KUTOKA KISWAHILI: MTAZAMO WA MLINGANO CHANZI

POLYCAP OKOTH ADICKA
C50/67102/2013

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2016

University of NAIROBI Library
0547853 2

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi: ………………………………………………………… Tarehe: 7/11/2016………

POLYCAP OKOTH ADICKA

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi: ………………………………………………………… Tarehe: 07/11/2016………

PROFESA IRIBE MWANGI

Sahihi: ………………………………………………………… Tarehe: 8·11·2016………

DAKTARI HANAH MWALIWA

# TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa nyanyangu Magdalina Oyare Mboya ambaye baraka zake zimenifikisha katika kiwango hiki.

Pili, ninaitabaruku kwa wazazi wangu Joseph Mboya na Gaudencia Adika pamoja na muhibu wangu Mercy Auma.

## SHUKRANI

Kukamilika kwa mradi huu kulitokana na juhudi za wengi. Hivyo, ninachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia kwa namna yoyote ile ili kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Kwa kutaja wachache, ninawashukuru wasimamizi wangu: Profesa Iribe Mwangi na Daktari Hanah Mwaliwa ambao hawakuchoka kunipa mwelekeo mwafaka, ushauri na mawaidha adimu ambayo yaliniwezesha kuiboresha na kuimarisha kazi hii.Natoa shukrani ghaya kwenu.

Hali kadhalika, nawashukuru wahadhiri katika Idara ya Kiswahili pamoja na Idara ya Isimu na Lugha kwa kunielekeza katika taaluma ya usomi tangu mwanzo wa kozi hii ya uzamili hadi mwisho. Maarifa mliyonipa kuhusu mada mbalimbali za isimu na fasihi yalifinyanga mawazo yangu kuhusu masuala ya kiakademia. Kwa hayo yote, sina budi kuwavulia kofia. Isitoshe, natoa shukrani kwa wanafunzi niliokuwa nao katika darasa la uzamili; walinihimiza na kunitia moyo katika mazingira yenye changamoto tele.

Shukrani zangu za mwisho ni kwa wazazi wangu ambao wamenitia moyo tangu nilipoanza masomo haya. Kutokana na ushauri mzuri walionipa, nimeweza kujikaza na kusonga mbele hadi tamati. Mwendani wangu Mercy Auma naye namshukuru kwa kunipa motisha ya kipekee katika safari hii ndefu ya kiakademia. Pia, siwezi kuwasahau wasimamizi wa shule ya upili Agoro Sare kwa kunipa mazingira mazuri ya kuendeleza kielimu. Miongoni mwao ni Mwalimu Mkuu Bw. Maurice Ogutu na manaibu wake; pamoja na walimu wengine wote. Nawashukuru sana.

Kutokana na upungufu wa wasaa, si rahisi kuwataja wote walionifaa kwa namna moja au nyingine ili kufanikisha kazi hii. Hata hivyo, ninakiri kuwa mchango huo ulikuwa na umuhimu wa kipekee katika kazi hii. Nawashukuru kwa dhati.

# IKISIRI

Utafiti huu ni uchunguzi wa utohozi wa nomino za lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini ambazo zimetoholewa kutokana na lugha ya Kiswahili. Nomino hizi za mkopo zimechanganuliwa ili kutathmini michakato ya kiutohozi inayotumiwa kwenye harakati za ukopaji wa maneno hayo (ya Kijaluo) kutoka lugha ya Kiswahili. Michakato hiyo inaangaziwa katika viwango viwili vya kiisimu: kiwango cha kifonolojia na kile cha mofolojia. Uchanganuzi huu unaongozwa na mkabala wa mlingano-chanzi ambao ni kimelea cha nadharia ya upeo. Nadharia hii inashikilia kuwa maumbo ya maneno-mkopo yanatokana na mtagusano baina ya kanuni zinazokinzana za lugha husika. Miongoni mwa kanuni hizo ni kanuni ya uaminifu ambao unasisitiza ulinganifu katika miundo ya nje ya vipande-sauti vya lugha-changizi na vile vya lugha-pokezi. Kanuni hii ndiyo uti wa mgongo wa mkabala wa mlingano-chanzi. Mkabala huu unafafanua mifanano iliyopo katika maumbo ya vipande sauti vya lugha-pokezi (Kijaluo) na vile vya lugha-changizi (Kiswahili). Matokeo yameonyesha kuwa ingawa mfanyiko wa utohozi huongozwa na mikakati mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia, kuna mfanano mkubwa kati ya lugha-pokezi na lugha-changizi. Hali hii inaelezeka kwenye mtazamo wa mlingano-chanzi kupitia kanuni yake ya uaminifu. Kifonolojia, taratibu za kiutohozi zilizobainishwa ni: udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji-sifa. Kwa upande mofolojia, utaratibu wa kiutohozi uliotamalaki kwenye utohozi wa maneno ya Kiswahili yanayoingia katika Kijaluo ni uambishaji.

## VIFUPISHO NA ALAMA

| <u>**KIFUPISHO/ ALAMA**</u> | <u>**MAANA**</u> |
|---|---|
| I | Irabu |
| K | Konsonanti |
| KI | Konsonanti-Irabu |
| V | Vokali |
| K-V | Konsonanti-Vokali |
| Kons | Konsonanti |
| Kif | Kifulizwa |
| Kikw | Kikwamizwa |
| LKNK | Lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini |
| *MAX – SB* | Kanuni kuwa vipande-sauti vyote katika neno-changizi viwe katika neno-pokezi. |
| *DEP – SB* | Kanuni kuwa vipande-sauti vyote katika neno-mkopo viwe katika neno-changizi. |
| [ ] | Unukuzi Kifonetiki |
| / / | Uwasilishaji wa Fonimu |
| { } | Uwasilishaji wa Mofu |
| $ | Mpaka wa Silabi |
| > | Badiliko kutoka Kiswahili kuelekea Kijaluo |
| # | Mpaka wa neno |
| Ø | Mofu kapa |

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1 Mifano ya Maneno ya Lahaja za Kijaluo

Kielelezo 2 Irabu za Kijaluo

Kielelezo 3 Jedwali la Uainisho wa Konsonanti za Kiswahili

Kielelezo 4 Unukuzi wa Irabu za Kijaluo Kiothografia/Kifonetiki

Kiekelezo 5 Jedwali la Uainisho wa Irabu za Kijaluo

Kielelezo 6 Jedwali la Fonimu za Kiswahili

Kielelezo 7 Jedwali la Uainisho wa Konsonanti za Kiswahili

Kielelezo 8 Mchoro wa Uainisho wa Fonimu za Irabu

Kielelezo 9 Jedwali la Ngeli za Kimofolojia za Kiswahili

YALIYOMO

UNGAMO .......... ii
TABARUKU .......... iii
SHUKRANI .......... iv
IKISIRI .......... v
VIFUPISHO NA ALAMA .......... vi
ORODHA YA VIELELEZO .......... vii
YALIYOMO .......... viii

SURA YA KWANZA .......... 1
UTANGULIZI .......... 1
1.1 Usuli wa Utafiti .......... 1
1.1.1 Lugha Zitakazoshughulikiwa .......... 3
1.1.1.1 Lugha ya Kijaluo .......... 4
1.1.1.2 Lugha ya Kiswahili .......... 5
1.2 Swala la Utafiti .......... 6
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 8
1.4 Nadharia Tete za Utafiti .......... 9
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 9
1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 11
1.7 Fasili za Istilahi .......... 13
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 14
1.8.1 Maandishi ya Kijumla Kuhusu Ukopaji Maneno .......... 15
1.8.2 Maandishi kuhusu Utohozi-mkopo katika Kijaluo .......... 18
1.9 Misingi ya Kinadharia .......... 21

1.9.1 Nadharia ya Upeo ..... 21
1.9.2 Mkabala wa Mlingano Chanzi ..... 22
1.10 Mbinu za Utafiti ..... 23
1.10.1 Ukusanyaji Data ..... 24
1.10.2 Utambuzi wa Maneno Mkopo ..... 25
1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ..... 25
1.11 Hitimisho ..... 27

**SURA YA PILI ..... 28**

**MISINGI YA KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA YA KIJALUO NA KISWAHILI ..... 28**

2.1 Utangulizi ..... 28
2.2 Fonolojia za lugha Zinazotafitiwa ..... 28
2.2.1 Fonolojia ya Kijaluo ..... 28
2.2.1.1 Konsonanti za Kijaluo ..... 29
2.2.1.2 Irabu za Kijaluo ..... 32
2.2.1.3 Silabi za Kijaluo ..... 33
2.2.1.4 Miundo ya Silabi za Kijaluo ..... 35
2.2.2 Fonolojia ya Kiswahili ..... 38
2.2.2.1 Konsonanti za Kiswahili ..... 40
2.2.2.2 Irabu za Kiswahili ..... 43
2.2.2.3 Silabi za Kiswahili ..... 44
2.2.2.4 Miundo ya Silabi za Kiswahili ..... 45
2.3 Mofolojia za Lugha Zinazotafitiwa ..... 49
2.3.1 Mofolojia ya Nomino za Kijaluo ..... 49
2.3.1.1 Uwingi wa Nomino katika Kijaluo ..... 50
2.3.1.2 Hali za Umilikaji katika Nomino za Kijaluo ..... 51

2.3.2 Mofolojia ya Nomino za Kiswahili ........ 52
2.4 Hitimisho ........ 54

**SURA YA TATU ........ 55**
**UTOHOZI WA KIFONOLOJIA ........ 55**
3.1 Utangulizi ........ 55
3.2 Utohozi wa Fonimu ........ 55
3.2.1 Utohozi wa Irabu ........ 56
3.2.2 Utohozi wa Konsonanti ........ 59
3.2.2.1 Udumishaji wa Konsonanti ........ 59
3.2.2.2 Ubadilishaji wa Konsonanti ........ 62
3.3 Utohozi wa Silabi ........ 66
3.3.1 Mifanyiko Inayohusishwa na Utohozi wa Silabi ........ 66
3.3.1.1 Udondoshaji ........ 66
3.3.1.2 Ubadili wa Silabi ........ 70
3.3.1.3 Uchopekaji ........ 71
3.4 Hitimisho ........ 74

**SURA YA NNE ........ 75**
**UTOHOZI WA KIMOFOLOJIA ........ 75**
4.1 Utangulizi ........ 75
4.2 Mikakati ya Utohozi wa Kimofolojia ........ 75
4.2.1 Viambishi vya Idadi katika Nomino Mkopo ........ 76
4.2.2 Viambishi vya Hali ya Umilikaji katika Nomino Mkopo ........ 80
4.3 Mifanyiko ya Utohozi wa Kimofolojia na Mkabala wa Mlingano Chanzi ........ 83

4.4 Hitimisho ........................................ 85

**SURA YA TANO ........................................ 86**

**MUKHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................ 86**

5.1 Utangulizi ........................................ 86

5.2 Mukhtasari wa Matokeo ........................................ 86

5.3 Tathmini ya Nadharia Tete na Matokeo ya Utafiti ........................................ 88

5.4 Hitimisho ........................................ 89

5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ........................................ 90

**MAREJELEO ........................................ 92**

**KIAMBATISHO ........................................ 96**

**MANENO-MKOPO YA KIJALUO KUTOKA KISWAHILI ........................................ 96**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Watafiti wamechunguza fonolojia na mofolojia za lugha mbalimbali ikiwemo lugha ya Kijaluo. Kati ya wale waliochunguza lugha ya Kijaluo ni pamoja na Adhiambo (1981), Okombo (1982), Owino (2003) na wengine. Tafiti hizi zimejikita katika ngazi za kiisimu za fonolojia na mofolojia ya Kijaluo kwa jumla au hata katika muktadha wa msamiati-mkopo. Wingi wa tafiti hizi zimejikita katika lahaja ya Nyanza Kusini kwani ndiyo inayotumiwa katika maeneo mengi zaidi nchini Kenya; lahaja nyingine ya Kijaluo ni ile ya Trans-Yala, ambayo pia huitwa lahaja ya Boro Ukwala (Suleh, 1995).

Maandishi juu ya tafiti zilizofanywa kuhusu utohozi wa kifonolojia na kimofolojia ya maneno-mkopo yanaonyesha kwamba tafiti hizo hazitambui kwamba tofauti za kilahaja zina mchango kwenye mchakato wa utohozi wa maneno-mkopo katika lugha ya Kijaluo. Badala yake, aghalabu inachukuliwa kuwa 'Kijaluo' na 'lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini' ni dhana moja kwenye mukhtadha wa utohozi wa msamiati-mkopo. Hii ni sawa na kunena kwamba michakato ya kiutohozi ya maneno mkopo inafanana katika lahaja zote mbili za Kijaluo. Chukulizi za aina hii hazizingatii kwamba ingawa kuna kuelewana baina ya lahaja hizi, lahaja zenyewe zinatofatiana katika vipengele maalum vya kiisimu: yaani matamshi na msamiati (Suleh, 1995). Tofauti hizi zinaweza kuathiri mkondo wa michakato ya kutohoa msamiati-mkopo. Kwa mfano, tukizingatia tofauti za kimsamiati, kuna baadhi ya maneno katika lahaja ya Trans-Yala ambayo mzawa wa lahaja ya Nyanza Kusini atatatizika pakubwa katika kutambua maana yao; hasa yasipotumiwa katika muktadha unaofaa. Kwa mfano, Oluoch (2014:8) anatambua msamiati ufuatao wa lahaja ya Nyanza Kusini pamoja na visawe vyao katika lahaja ya Trans-Yala:

**Kielelezo 1: Mifano ya Maneno ya Lahaja za Kijaluo**

| **Lahaja ya Nyanza Kusini** | **Lahaja ya Trans-Yala** | **Maelezo kwa Kiswahili** |
|---|---|---|
| Raura | Rasingwa | Mjinga |
| Pi kuon | Hawarha | Maji yaliyochemshwa ili kupika ugali |
| Puodho | Ndalo | Shamba |
| Oluth kuon | Oliho | Mwiko |

Maneno katika safu ya lahaja ya Trans-Yala (kwenye jedwali) hayatatambuliwa kabisa na mzawa wa lahaja ya Nyanza Kusini iwapo hayatajitokeza katika muktadha sahihi. Sababu ni kwamba, maneno haya yametokana na mtagusano baina ya lahaja ya Kijaluo ya Trans-Yala na lugha jirani ya Kiluhyia, kama vile lahaja za Kilumarachi na Kilunyala (Oluoch, 2014). Lahaja hizi za Kiluhyia hazijatagusana na lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini kwa njia yoyote ile kwa sababu ya umbali wa kimaeneo. Mtagusano huo pia umeingiza vipengele vigeni vya kiisimu katika lahaja ya Trans-Yala na kuufanya utofautiane na ile lahaja nyingine ya Nyanza Kusini. Ni katika misingi hii ambapo utafiti huu ulikusudia kutathmini michakato ya utohozi wa msamiati-mkopo (unaotokana na Kiswahili) katika lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini kwenye mkabala wa Mlingano Chanzi bila kuihusisha lahaja hii na ile ya Trans-Yala. Sababu ni kuwa, lahaja hizi mbili zinaingiliana na lugha zingine katika mazingira ya kiisimu yaliyotofauti.

Mtazamo huu ni tofauti na ule wa watafiti kama vile Oluoch (2014) ambaye alichunguza fonolojia na mofolojia ya maneno-mkopo katika lahaja ya Kijaluo ya Trans-Yala (maneno yaliyokopwa kutokana na lahaja za Kiluhyia na Kiswahili) japo alihusisha lahaja zote mbili za Kijaluo. Pia, mwelekeo huu wa kiuchunguzi unatofautiana na ule wa Owino (2003) ambaye

alichunguza fonolojia ya maneno mkopo ya Kijaluo (kutokana na Kingereza na Kiswahili) *ingawa aliongozwa nadharia ya fonolojia vipande-sauti (auto-segmental phonology)* na *fonolojia* ya konsonanti-irabu *(C-V phonology).*

Uchunguzi wetu wa yaliyoandikwa kuhusu tafiti ambazo zimefanywa juu ya msamiati-mkopo katika lugha ya Kijaluo ulionyesha kuwa hakuna utafiti wowote ambao umefanywa kuhusu fonolojia/mofolojia ya maneno-mkopo katika lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini (msamiati unaotokana na lugha ya Kiswahili) ukiongozwa na Mkabala wa Mlingano Chanzi *(Source-Similarity Model).* Kwa hivyo, utafiti huu ni ada kubwa kwa watafiti/wataalamu katika taaluma ya isimu na utohozi wa maneno-mkopo kwenye lahaja hii ya Kijaluo ya Nyanza Kusini.

### 1.1.1 Lugha Zilizoshughulikiwa

Lugha ambazo zilichunguzwa katika utafiti huu ni mbili: lugha ya Kijaluo (lahaja ya Nyanza Kusini) na lugha ya Kiswahili. Katika Kijaluo, lahaja ya Nyanza Kusini iliteuliwa kwa vile uchunguzi wetu ulionyesha kuwa hakuna utafiti wa kina uliokuwa umefanywa kuhusu fonolojia na mofolojia ya msamiati mkopo katika lahaja hii katika Mkabala wa Mlingano Chanzi *(source similarity model).* Pia, lahaja hii ya Kijaluo ndiyo lugha ya kwanza ya mtafiti. Hivyo, mtafiti ana umilisi na utendaji wa viwango vya kutosha katika lugha yenyewe; pia aliweza kuitumia pakubwa katika madarasa ya mwanzo ya shule za msingi. Kiswahili nacho kiliteuliwa kwa vile mtafiti ni msomi na mtaalamu wa lugha hii. Zaidi ni kwamba, Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya pamoja na kuwa somo la lazima katika shule za msingi na upili nchini Kenya (anakotoka mtafiti). Pia, ujuzi wa mtafiti wa lugha zinazotafitiwa katika uchunguzi wa kiisimu ni kipengele muhimu katika kufanikisha utafiti wenyewe; huu ndio ulikuwa msingi wa kuchagua Kijaluo na Kiswahili katika utafiti huu.

#### 1.1.1.1 Lugha ya Kijaluo

Kijaluo ni lugha inayotumiwa na watu wanaoitwa Wajaluo ambao wanapatikana nchini Kenya, Uganda pamoja na Tanzania yote yakiwa ni maeneo ya Afrika Mashariki. Lugha hii ni mojawapo ya lugha zinazounda kundi pana la lugha ambazo kwa pamoja zinarejelewa kama lugha za Kiniloti.Kwa uhakika, Kijaluo kinapatikana miongoni mwa lugha za Kiniloti za Magharibi. Lugha zingine ambazo zinapatikana katika kundi hili ni pamoja na Kiacholi, Kilang'o, Kialur na Kipadhola; wazungumzaji wa awali wa lugha hizi walihama kutoka eneo la Sudan Kusini na kutapakaa katika janibu za Kenya, Uganda na Tanzania (Ochieng', 1985).

Kulingana na Cohen (1974), Wajaluo walianza kuishi katika maeneo ya Magharibi ya Kenya (Nyanza) mnamo miaka ya 1500-1550 Baada ya Kristo. Eneo hilo ambalo lilirejelewa kama mkoa wa Nyanza sasa limegawanywa katika kaunti nne: Migori, Homa-Bay, Siaya na Kisumu. Isitoshe, Wajaluo pia wanapatikana katika nchi za Tanzania na Uganda. Kwa mujibu wa takwimu za idadi ya watu nchini Kenya (2009), Wajaluo walikuwa takriban watu milioni nne. Hata hivyo, takwimu hizi hazikujumuisha wale Wajaluo wanaoishi nchini Uganda na Tanzania.

Stafford (1967) anadokeza kuwa Kijaluo kina lahaja mbili kuu: lahaja ya Trans-Yala (pia huitwa lahaja ya Boro-Ukwala) na lahaja ya Nyanza Kusini. Lahaja ya Trans-Yala inatumiwa katika kaunti ya Siaya kwenye maeneo kama vile Ugenya, Alego, Yimbo pamoja na sehemu za Gem. Lahaja ya Nyanza Kusini nayo inatumiwa katika eneo la Nyanza Kusini (kaunti za Homa-bay na Migori), pamoja na maeneo ya kaunti za Siaya na Kisumu ambayo hayakutajwa katika orodha ya maeneo yanayotumia lahaja ya Trans-Yala. Owino (2003) anadokeza kwamba lahaja ya Nyanza Kusini ndiyo inayotumiwa kama lahaja sanifu na ndiyo inayotumiwa kwa wingi katika maandishi ya Kijaluo. Kwa sababu hiyo, utafiti huu umejikita katika lahaja ya Nyanza Kusini. Kiuchumi, Wajaluo wanashiriki katika ukulima, uvuvi pamoja na ufugaji. Vipengele hivyo vya

kiuchumi ndivyo ambavyo ni msingi wa mtagusano baina ya Wajaluo na wazungumzaji wa lugha zingine nchini Kenya (miongoni mwao wakiwemo wazungumzaji wa Kiswahili). Kwa mfano, Kiswahili kinatumika katika mawasiliano ya kibiashara baina ya Wajaluo na wazungumzaji wa lugha zingine za kikabila nchini Kenya.

#### 1.1.1.2 Lugha ya Kiswahili

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kibantu. Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na Guthrie (1962), Kiswahili kiliwekwa katika kundi la lugha za Kibantu na kwamba kulikuwa na ishara za kuzungumzwa kwa lugha hii kwenye maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya karne ya kumi. Kwa mujibu wa Polome (1967: 9), neno 'Kiswahili' lina asili yake katika neno la Kiarabu 'sawahil' (kwa wingi: 'sahil') lenye maana ya 'pwani'. Wazungumzaji wa Kiswahili nao wakarejelewa kama 'Waswahili'. Kutokana na dhana kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu, chimbuko lake ni sawa na lile la lugha zingine za Kibantu; asili ya lugha za Kibantu ni maeneo ya Kongo. Historia inaonyesha kuwa Waswahili walienea katika maeneo mbalimbali ya Afrika yakiwemo Pwani ya Afrika Mashariki.

Polome (1967), anasema kuwa pamoja na maeneo ya Afrika Mashariki, Kiswahili pia kinazungumzwa katika janibu za Afrika ya Kati, Afrika Kusini, eneo la Kusini mwa Oman kule Uajemi. Anazidi kufafanua maingiliano baina ya Waswahili na wageni kutoka nchi zingine ambapo anadai kuwa rekodi za kihistoria kama vile Tarihi za Kilwa zinaonyesha mangiliano baina yao na wageni. Maingiliano hayo yanaibuka katika miktadha ya dini, biashara, ndoa, utawala na mengineyo. Baadaye, ukoloni ulipokita mizizi kwenye maeneo haya ya Afrika Mashariki katika karne ya kumi na tisa, Kiswahili kilitekeleza wajibu muhimu kwani kilitumika katika kufanikisha shughuli za kikoloni hasa zile za kiutawala.Isitoshe, pia kilitumika kutekeleza majukumu ya kielimu.

Takwimu za makadirio zinaonyesha kuwa wazungumzaji wa Kiswahili ni kati ya milioni 50 na 70; wengi wakiwa wanaitumia kama lugha yao ya pili (Campbell, 1991: 1283). Kiswahili pia ni *lingua franka* ya Afrika Mashariki na Kati. Zaidi ni kwamba, Kiswahili kimepewa hadhi ya juu katika eneo la Afrika Mashariki. Nchini Kenya kwa mfano, Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi; hivyo ndivyo ilivyo pia katika nchi ya Tanzania. Kwenye elimu, lugha ya Kiswahili imepewa nafasi teule kwani ni somo la kutahiniwa katika viwango vya shule za upili na msingi katika nchi za Afrika Mashariki (Iribemwangi na Mukhwana, 2011).

Kiswahili pia kina lahaja zake ingawa wataalamu wametofautiana kuhusu idadi kamili ya lahaja zenyewe. Lahaja hizi zimetapakaa katika maeneo ambapo lugha hii inatumiwa. Polome (1967:19) anatambua lahaja kumi na tano anazorejelea kama lahaja za pwani na visiwani. Miongoni mwa lahaja hizo ni pamoja na Chimiini, Kipate, Kitumbatu, Kisiu, Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kimtang'ata na nyinginezo. Pia, anatambua lahaja za bara ambazo ni lahaja za kijamii. Lahaja hizo ni pamoja na Kisettla, Kishamba, Kihindi na Kivita. Pia, kuna lahaja ya Kiswahili Sanifu ambayo ndiyo hutumiwa katika miktadha ya kielimu pamoja na miktadha mingine iliyo rasmi.

## 1.2 Swala la Utafiti

Lugha mbili zinapoingiliana kimatumizi, huwa ni kawaida kuathiriana. Kuathiriana kule kunaweza kuleta mabadiliko katika lugha zilizohusika. Hata hivyo, athari nyingi hutokea katika upande wa msamiati ambapo wazungumzaji wa lugha hizo wanaweza kukopana msamiati. Hali hii hutokea kwa sababu ya kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za ulimwengu kutokana na ukuaji wa maendeleo kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa na kijamii (Iribemwangi & Mukhwana, 2011:156). Mara nyingi msamiati kutoka lugha moja (unaokopwa na lugha nyingine) hupitia mifanyiko anuwai ambayo hulenga kuyapatia maneno-mkopo muundo ambao unakubalika

katika lugha pokezi. Hata hivyo, katika harakati za kuyapatia maneno-mkopo maumbo yanayokubalika katika lugha pokezi, lugha pokezi hujitahidi kudumisha mfanano kwa kiwango fulani na neno lililokopwa (la lugha changizi).

Utafiti huu basi ulikusudia kubainisha michakato ya kifonolojia na kimofolojia ambayo neno la Kiswahili hupitia katika harakati za ukopaji wa msamiati ili liweze kukubaliwa kama neno kamili la Kijaluo. Katika mchakato huu wa utohozi, ilidhihirika kwamba, lugha pokezi hujaribu kadri inavyowezekana kudumisha sifa mbalimbali za kimaumbo zinazojitokeza katika lugha changizi; sifa ambazo ni za maneno ya lugha changizi (ambayo yanakopwa).

Kumetokea athari baina ya Kiswahili na lugha za kienyeji nchini Kenya kutokana na hadhi ya Kiswahili ya kuwa lugha ya taifa la Kenya. Kwa mfano, Mudhune (2008) anapochunguza athari za Kijaluo miongoni mwa wanaojifunza Kiswahili, anabaini kuwa Kijaluo huathiri Kiswahili mzungumzaji anapoingiza vipengele vya fonolojia ya Kijaluo katika lugha ya Kiswahili; hasa sauti za Kiswahili zisizopatikana katika Kijaluo. Kijaluo ni mojawapo ya lugha zilizoathiriwa na mtagusano huu kwani msamiati unaotokana na Kiswahili umeweza kuingizwa katika Kijaluo. Fikra hii inalingana na wazo la Thompson (2001) anayedokeza kuwa athari ya kawaida zaidi ya mtagusano baina ya lugha tofauti ni ukopaji wa maneno. Msamiati-mkopo unapoingia katika lugha, mambo mawili huweza kutokea: neno linalokopwa huweza kufanyiwa marekebisho ya kifonolijia/kimofolojia ama libaki bila mageuzi yoyote. Kwa hivyo, mtafiti alishughulikia namna ambavyo mzungumzaji asilia wa Kijaluo hutohoa msamiati kutoka lugha ya Kiswahili na kuufanya uingie katika mfumo wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini.

Kwa mfano, lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini ina msamiati kama ufuatao (unaotokana na lugha ya Kiswahili): *okombe* [okombe] kutokana na 'kikombe', *sufria* [sufrIa] kutokana na 'sufuria', *ogunia* [ogunia] kutokana na 'gunia', *makas* [makas] kutokana na 'makasi' na

kadhalika. Hapa, inadhihirika kwamba kuna mabadiliko yaliyofanyiwa msamiati wa Kiswahili kimaksudi ili uweze kuchukua mfumo wa kifonolojia na kimofolojia wa Kijaluo. Hata hivyo, bado kunabakia mfanano fulani kati ya msamiati wa lugha pokezi (Kijaluo) na ule wa lugha changizi (Kiswahili). Hali hii ndiyo uchunguzi huu unalenga kuweka wazi katika Mkabala wa Mlingano Chanzi *(Source Similarity Model).*

Katika kutimiza lengo la kubainisha mikakati inayopitiwa na maneno-mkopo kutoka Kiswahili, mabadiliko ya kisauti na kisilabi yalitiliwa maanani huku ikizingatiwa kwamba vipashio hivi ndivyo hupokea mageuzi mengi zaidi wakati wa utohozi. Isitoshe, mifumo ya mofimu zinazoandamana na msamiati wa Kijaluo wenye asili ya Kiswahili pia ilizingatiwa kwenye utafiti huu.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo yafuatayo:

i. Kuchanganua mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia inayopitiwa na maneno-mkopo kutoka lugha ya Kiswahili ili yaingie katika mfumo wa kawaida wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini (LKNK) katika Mkabala wa Mlingano Chanzi.

ii. Kuchanganua mifanyiko mbalimbali ya kimofolojia inayopitiwa na maneno-mkopo ya Kiswahili ili yaingie katika mfumo wa kawaida LKNK katika Mkabala wa Mlingano Chanzi.

iii. Kutathmini ulinganifu wa kifonolojia na kimofolojia uliopo baina ya msamiati-mkopo wa Kijaluo (uliokopwa kutokana na lugha ya Kiswahili) na msamiati asilia wa Kiswahili (ambao ndio unaokopwa). Ulinganishaji huu utazingatia vipengele vya kifonolojia na kimofolojia.

## 1.4 Nadharia Tete za Utafiti

i. Maneno-mkopo kutoka Kiswahili yanapitia michakato anuwai ya kifonolojia kabla ya kutambuliwa kama msamiati wa LKNK.

ii. Maneno-mkopo kutoka Kiswahili yanapitia michakato mbalimbali ya kimofolojia kabla ya kuingizwa katika mfumo wa LKNK.

iii. Kuna ulinganifu wa kifonolojia na kimofolojia baina ya msamiati-mkopo wa LKNK (unaotokana na lugha ya Kiswahili) na msamiati asilia wa Kiswahili uliokopwa.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika masuala yafuatayo: kwanza, ulishughulikia mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia inayopitiwa na msamiati wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini (uliotoholewa kutokana na lugha ya Kiswahili), kabla ya kutambuliwa na wazungumzaji wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini kama neno la kawaida la lahaja hiyo. Uchanganuzi huo ulijikita katika viwango viwili vya kiisimu: fonolojia na mofolojia. Kwa vile Kiswahili ni lugha ya Kibantu nayo Kijaluo ni lugha ya Kiniloti, uchanganuzi ulilenga mageuzi ya kifonolojia na kimofolojia ambayo neno la Kibantu hupitia ili neno lenyewe liweze kuingia kwenye mfumo wa LKNK.

Hii inatokana na dhana kwamba kuna tofauti bainifu za kiisimu kati ya lugha za Kibantu na zile za Kiniloti. Uchanganuzi wa mchakato wa ukopaji-msamiati ulitekelezwa kwa kuzingatia vipengele mahususi vya kifonolojia vipande-sauti ambavyo ni fonimu na silabi.

Hali kadhalika, utafiti huu ulichunguza (kwa mtindo wa kulinganisha) msamiati ambao ni tokeo la utohozi (msamiati wa lugha pokezi) na kuulinganisha na msamiati asilia wa lugha changizi. Nia ya uchunguzi wa aina hii ulikuwa ni kubainisha ulinganifu uliopo baina ya pande hizo mbili za maneno. Utaratibu huu uliongozwa na Mkabala wa Mlingano Chanzi.

Utafiti huu ulikuwa wa kisinkroniki wala si wa kidaikroniki kwani haukuangazia mabadiliko katika maneno-mkopo ambayo yametokea katika mpito wa wakati. Isitoshe, kiini cha ukopaji wa msamiati mahususi pia hakikushughulikiwa. Zaidi ni kuwa, msamiati uliochunguzwa ulikuwa ni ule uliokaotokana na vikoa teule vya kisemantiki pekee. Vikoa hivyo ni: uchukuzi, teknolojia, mawasiliano, biashara, utawala, afya, mazingira, ukulima, vyakula, mavazi, elimu, pamoja na vyombo vya kinyumbani/jikoni. Hii ni kusema kuwa msamiati-mkopo uliopo nje ya vikoa hivi haukushughulikiwa.

Hali kadhalika, kategoria ya nomino pekee ndiyo iliyoshughulikiwa kwani leksimu nyingi zinazokopwa katika lugha huwa ni nomino kwa vile kategoria hii ni wazi zaidi ikilinganishwa na zingine (Iribemwangi, 2013). Sababu nyingine ya kuteua kategoria ya nomino ni kuwa kujumuisha kategoria zote za maneno kungepanua mipaka ya utafiti kupita kiasi hivyo kutatiza utaratibu mzima wa utafiti kwa kuufanya uwe changamano kupita kiasi.

Masuala mengine ambayo hayakuangaziwa ni kama vile sifa za kifonolojia arudhi za lugha husika. Sababu ni kuwa vipengele vya fonolojia arudhi katika Kijaluo ni vingi na changamano mno kiasi cha kwamba haingewezekana kuvichanganua kikamilifu katika muda uliotengewa utafiti huu. Pia, utafiti haukushughulikia tofauti katika msamiati-mkopo ambazo zinatokana na tofauti za kilahaja katika lugha ya Kijaluo. Badala yake, utafiti huu ulijikita katika maneno-mkopo katika lahaja moja pekee ya Kijaluo: lahaja ya Nyanza Kusini kama inavyotumiwa na wazungumzaji wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini (LKNK) katika nchi ya Kenya, Kaunti ya Homa-bay, Wilaya ya Rachuonyo Kaskazini. Lugha ya Kijaluo inazo lahaja mbili kuu: Lahaja ya Trans-Yala na Lahaja ya Nyanza Kusini (Stafford, 1970). Kwa hivyo, katika utafiti huu, 'Kijaluo' kilitumika kwa maana ya 'lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini'.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa lugha ya Kiswahili kwani unadhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili imeathiri lugha zingine hasa katika muktadha wa nchi ya Kenya. Athari hizo zinaonekana katika kitengo cha msamiati ambapo lugha zinazotagusana na Kiswahili kama vile Kijaluo zinakopa leksimu (kutokana na lugha ya Kiswahili). Hali hii ilidhihirika waziwazi tulipochanganua mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia yanayotokea kwenye mchakato wa utohozi wa msamiati wa Kiswahili kabla ya kuingizwa katika LKNK.

Pili, uchanganuzi wa fonolojia na mofolojia ya msamiati uliokopwa ni muhimu kwani unafanikisha harakati za kuelewa muundo wa ndani wa lugha pokezi. Manufaa yake ni kuwa wanaisimu watazidi kuelewa sarufi za lugha za kiasili za Kiafrika huku ikizingatiwa kuwa lugha hizi hazijapewa nafasi kubwa katika mifumo ya elimu ikilinganishwa na lugha za kigeni. Hii inatokana na wazo kwamba uamilifu wa baadhi ya kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha hudhihirika wazi zaidi kanuni zenyewe zinapotumika kugeuza msamiati wa lugha nyingine ili uweze kuingia katika mfumo wa lugha-pokezi. Kwa hivyo, uchunguzi huu utapanua uelewa wa kanuni mbalimbali za kifonolojia na kimofolojia za lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini. Matokeo yake ni kuongeza maarifa zaidi juu ya yale yaliyotokana na chunguzi za awali kama vile ule wa Adhiambo (1981), alioyeangazia mifanyiko ya kifonolojia inayohusishwa na irabu za Kijaluo; Okombo (1982), ambaye alishughulikia fonolojia na mofolojia ya Kijaluo; Owino (2003) aliyeangazia fonolojia ya msamiati wa Kijaluo uliokopwa kutoka Kingereza na Kiswahili miongoni mwa tafiti zingine.

Pia, utafiti huu unaweza kuwafaidi walimu wa lugha ya Kiswahili kwani wanaweza kuutumia kuelewa matatizo yanayoweza kuwakabili wanafunzi Wajaluo wanaojifunza lugha ya Kiswahili;

hasa matatizo yale yanayotokana na lugha ya kwanza. Haya ni matatizo yanayotokana na mtagusano baina ya lugha yao ya kwanza (Kijaluo) na lugha ya Kiswahili.

Hali kadhalika, uelewa wa mchakato wa utohozi ni muhimu kwa kuwa unadhihirisha namna ambavyo msamiati mpya huingia katika lugha mahususi. Kutokana na umuhimu wa suala hili, wataalamu wamejaribu kuchanganua lugha kwa madhumuni ya kupata ufahamu wa kina kuhusu utaratibu wa utohozi. Hivyo basi, utafiti huu unaongeza maarifa kwenye harakati hizi za kutaka kuelewa mchakato mzima wa utohozi hasa katika muktadha wa lugha za Kiafrika, yaani Kiswahili na Kijaluo. Maarifa ya aina hiyo yatawafaa watafiti na wasomi wa baadaye ambao wangependa kufahamu mengi zaidi kuhusu utohozi hasa katika lugha ya Kijaluo.

Hali kadhalika, hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu utohozi-mkopo wa msamiati wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini (zenye asili katika lugha ya Kiswahili) kwa kutumia Mkabala wa Mlingano Chanzi. Hii ni kwa mujibu wa uchunguzi ambao tulifanya kwa kupitia maandishi mbalimbali juu ya tafiti za awali zilizofanywa kwa kutumia mkabala wa Mlingano Chanzi. Mkabala wa Mlingano Chanzi ndio ulikuwa msingi wa utafiti huu. Kwa hivyo, uchunguzi huu ni muhimu kwa vile ulitathmini ufaafu wa Mkabala wa Mlingano Chanzi kama msingi wa kufafanua mchakato wa ukopaji-maneno katika lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini. Matokeo yake ni kuwa wataalamu wengine wa baadaye wenye nia ya kufanya uchunguzi wa aina hii katika lugha zingine wataweza kutumia matokeo ya utafiti huu kama msingi wao.

Zaidi ni kuwa, watu wanaojifunza lugha ya Kijaluo kwa mara ya kwanza pia wanaweza kufaidika kutokana na utafiti huu. Sababu ni kwamba, wataweza kutumia data zilikazotokana na utafiti huu kurekebisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia ambayo wanaweza kutokea katika harakati zao za kujifunza lugha ya Kijaluo. Isitoshe, wanaofanya tafsiri na ukalimani (kutoka lugha zingine kwenda Kijaluo) pia wataweza kunufaika kutokana na uchunguzi huu kwani

utohozi ni mojawapo ya mikakati inayoweza kutumiwa katika taratibu za tafsiri au ukalimani. Wanaoweza kufaidika kwa namna hii ni kama vile wataalamu wanaotafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kuelekea lugha ya Kijaluo. Kwingineko, watumiaji wa Kijaluo katika kazi zingine kama vile utangazaji kwenye redio na uana-habari kwa jumla nao wanaweza kubaini utaratibu mwafaka wa kutohoa msamiati mgeni unaoingia katika lugha ya Kijaluo.

### 1.7 Fasili za Istilahi

**(a) Ukopaji-maneno**

Huu ni utaratibu wa kuchukua kipengele cha kileksika kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine ambayo ndiyo lugha pokezi. Kipengele hicho kinaweza kutumika katika lugha pokezi jinsi kilivyo au hata kufanyiwa mabadiliko ili kiweze kufuata masharti ya kifonolojia ya lugha hiyo.

**(b) Neno-mkopo**

Kipengele cha kileksika ambacho kinaingia katika lugha mahususi kupitia utaratibu maalum wa kiisimu; aghalabu muundo wake huwa na vipande-sauti vya lugha changizi. Kinaweza kufanyiwa mabadiliko maalum kabla ya kuingizwa katika lugha inayokopa neno au kuingizwa kwenye lugha inayokopa neno bila badiliko lolote.

**(c) Lugha-changizi**

Hii ni lugha inayotoa kiungo cha kileksika ambacho kinakopwa na lugha nyingine na hatimaye kutumika kama kipengele cha kileksika cha lugha hiyo nyingine (lugha pokezi).

**(d) Lugha-pokezi**

Lugha inayopata kipengele cha kileksika kutoka lugha nyingine kupitia mfanyiko wa ukopaji-maneno.

**(e) Neno-changizi**

Hili ni neno linalokopwa kutoka lugha maalum na kuingizwa katika mfumo wa lugha nyingine (lugha pokezi). Linaweza kupitia mabadiliko ya kifonolojia/kimofolojia kabla ya kuingizwa katika lugha pokezi.

**(f) Utohozi**

Mchakato wa kubadilisha kipengele cha kileksimu kilichokopwa kutoka lugha nyingine na kukifanya kifuate kanuni za kifonolojia/kimofolojia za lugha pokezi.

**(g) Kanuni ya Uaminifu**

Haya ni masharti ya Mkabala wa Mlingano Chanzi yanayosisitiza kuwepo kwa mfanano baina ya vipengele vya kileksika vya lugha changizi na vile vya lugha pokezi katika mchakato wa utohozi wa maneno-mkopo. Kwa mujibu wa masharti haya, vipengele vyote katika lugha changizi viwe kwenye lugha pokezi.

**(h) *Lingua franka***

Lugha inayotumiwa katika eneo pana kijiografia na watu waliogawanyika kilugha ili kurahisisha mawasiliano na pia kuwaunganisha.

## 1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mengi yameandikwa kuhusu mada ya ukopaji wa maneno. Kuna maandishi yanayohusiana na ukopaji maneno kwa jumla na pia kuna yale yanayohusu ukopaji-maneno katika lugha ya Kijaluo kutokana na lugha zinazoingiliana nayo. Makundi haya mawili yanatupatia vijisehemu viwili vya yaliyoandikwa kuhusu mada:

i. Maandishi ya kijumla kuhusu ukopaji maneno

ii. Maandishi kuhusu utohozi-mkopo katika Kijaluo

### 1.8.1 Maandishi ya Kijumla Kuhusu Ukopaji Maneno

Dhana ya ukopaji-maneno imeelezwa na wataalamu mbalimbali. Kwa mfano, Crystal (1987) anafafanua ukopaji-maneno kama mkakati wa kuingiza neno au vipengele vingine vya kiisimu katika lugha maalum; aghalabu vipengele kama hivi hutokana na lugha au lahaja zingine. Maneno ambayo yanaingia katika lugha fulani kwa njia hii ndiyo hurejelewa kama 'maneno-mkopo'.

Ukopaji wa maneno hutokana na mtagusano baina ya lugha tofauti (Arlotto, 1972). Mtagusano wa aina hii ndio ubadilishanaji wa maneno katika vikoa mbalimbali vya kisemantiki. Kwa hivyo, ukopaji-maneno hujaza pengo fulani la kimaana katika lugha pokezi. Dhana hii ni ya kimsingi kwani katika utafiti huu, tutabainisha vikoa vya kisemantiki vya lugha ya Kijaluo ambavyo vina mapengo ambayo ndiyo yanajazwa kupitia maneno-mkopo. Baadhi ya vitengo vya maana vyenye maneno-mkopo ni pamoja na: elimu, upishi, uchukuzi, biashara, ukulima, vyombo vya nyumbani na utawala.

Iribemwangi na Mukhwana (2011:156) wanasema kwamba ukopaji wa maneno hutokana na kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za kilimwengu kutokana na ukuaji wa kimaendeleo. Hii ni kumaanisha kuwa lugha sharti iwe na mikakati teule ambayo itatumika ili kubuni msamiati mpya wa kurejelea dhana kama hizo. Njia mojawapo ya kuunda maneno mapya ni kukopa na kutohoa. Kwa mujibu wa waandishi hawa, ukopaji wa maneno huandamana na ugeuzaji wa maneno ili yaweze kufuata kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi. Ugeuzaji huu ndio huitwa utohozi.

Utohozi huwezesha lugha-pokezi kujiepusha na hatari ya kujilemaza kwa miundo mipya inayotokana na lugha changizi (Iribemwangi na Mukhwana, 2011:157). Wazo hili ni muhimu katika utafiti huu kwani tutaweza kubainisha jinsi ambavyo lugha ya Kijaluo inavyokabili mifumo migeni ya msamiati uliokopwa kutokana na lugha ya Kiswahili na kuibadilisha ipasavyo ili iweze kuoana na ruwaza ya kifonolojia na kimofolojia ya Kijaluo.

Kwingineko, Kenstowizs na Suchato (2006) wanatambua kwamba utohozi wa msamiati-mkopo unahusisha marekebisho yanayoongozwa na masharti. Wanashikilia kwamba, katika hali halisi kwenye mchakato wa kutohoa maneno-mkopo, mzungumzaji huwa na nia ya kudumisha uaminifu kwa lugha changizi na wakati huo kufanya maneno-mkopo kuwa na ruwaza ya vipande-sauti na sifa arudhi ambazo zinakubalika katika lugha pokezi. Uaminifu unaorejelewa hapa ni uhifadhi wa sifa za kifonolojia zinazojitokeza katika lugha changizi; yaani sifa hizi zijitokeze katika lugha pokezi kadri inavyowezekana. Maoni haya yatafaa sana katika uchunguzi huu kwa vile utafiti huu unalenga kudhihirisha mabadiliko yanayofanyiwa msamiati wa Kiswahili (ambao unaingizwa katika lugha ya Kijaluo) huku ikijaribu kudumisha ruwaza ya kifonolojia ya lugha changizi (ambayo ni Kiswahili).

Kwa upande mwingine, Karuru (2012) anachunguza utohozi wa kifonolojia na kimofolojia wa maneno-mkopo ya Gi-Gichugu (lahaja ya Gikuyu) ambayo yanatokana na Kingereza na Kiswahili kwa kutumia Mkabala wa Mlingano Chanzi. Uchunguzi huu unadhihirisha kwamba Gi-Gichugu hutumia michakato anuwai katika kutohoa maneno-mkopo kutoka lugha ya Kiswahili na Kingereza. Michakato hiyo ni pamoja na uambishaji, udondoshaji, uchopekaji na nyinginezo. Hata hivyo, maneno yaliyokopwa hujitahidi kufanana kifonolojia na maneno ya lugha changizi.

Ingawa lugha ambazo zilichunguzwa na Karuru (2012) ni tofauti na zile zilizotafitiwa hapa, uchunguzi huo una umuhimu kwetu kwani nadharia ambayo ilitumiwa (Mkabala wa Mlingano Chanzi) ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Isitoshe, vipengele vya kiisimu vilivyoangaziwa kwenye utafiti huo (fonolojia na mofolojia) ndivyo vilitiliwa maanani katika ukopaji wa msamiati katika lugha ya Kijaluo.

Lehman (1975) kwa upande wake anafafanua namna ambavyo ukopaji-maneno huweza kuathiri mifumo ya kifonolojia ya lugha pokezi. Anasema kuwa ukopaji-maneno katika lugha ya Kingereza (kutokana na lugha ya Kifaransa na Kirusi) umeathiri ruwaza ya kifonolojia ya Kingereza kwa vile sauti geni zimeweza kuingizwa katika lugha ya Kingereza. Sauti hizo ni pamoja na /ʤ/ na /sk/ ambazo kiasilia si sauti za lugha ya Kingereza. Katika utafiti huu, tutatathmini iwapo hali kama hii imetokea katika lugha ya Kijaluo kwenye harakati zake za kukopa msamiati kutoka lugha ya Kiswahili.

Mwaliwa (2014) naye anachanganua miundo ya silabi za maneno ya Kiswahili Sanifu yaliyokopwa kutoka Kiarabu Sanifu ya Kisasa pamoja na marekebisho yanayoandamana mchakato huo. Uchunguzi wenyewe unaongozwa na nadharia ya fonolojia zalishi ya konsonanti-vokali (*Generative C-V Phonology).* Anabainisha michakato ya kifonolojia inayoelekeza utohozi wa msamiati-mkopo wa Kiswahili Sanifu kutoka Kiarabu Sanifu ya Kisasa. Michakato yenyewe inasukumwa na kanuni za miundo ya silabi, vipengele vya kifonimu, kanuni za usilimisho pamoja na vigezo vya kimofolojia. Isitoshe, anabainisha kuwa maneno mengi hutoholewa ili yapate mifumo ya silabi inayopendelewa na Kiswahili Sanifu.Hata hivyo, kuna mengine machache yanayoingizwa bila kufanyiwa mabadiliko yoyote. Matokeo ya hali hii ni kuchipuka kwa vipengele vigeni vya kifonojia na kimofolojia katika mfumo wa Kiswahili Sanifu.

Kuna tafiti zingine nyingi ambazo pia zinagusia utohozi wa maneno-mkopo. Kwa mfano, Mbonankira (2004), ambaye anashughulikia utohozi wa msamiati wa Kiswahili na Kingereza kuingia lugha ya Kinyarwanda; Kimani (2005), anayeangazia utohozi wa msamiati-mkopo kutoka lugha ya Gikuyu kuingia lugha ya Kimasai miongoni mwa nyingine. Hata hivyo, zile ambazo zina umuhimu wa kipekee katika utafiti wetu ndizo zimezingatiwa kwa undani zaidi.

### 1.8.2 Maandishi kuhusu Utohozi-mkopo katika Kijaluo

Kuna maandishi mengi ya kiutafiti ambayo yanahusiana na ukopaji-msamiati pamoja na utohozi katika lugha ya Kijaluo. Kwa mfano, Owino (2003) anachanganua fonolojia ya maneno-mkopo ya Kijaluo kutoka Kingereza na Kiswahili. Utafiti wake unaangazia utohozi mkopo katika viwango vya fonimu, ruwaza ya silabi na sifa arudhi. Kwa hivyo, anaonyesha mageuzi ambayo hufanyiwa sauti geni katika harakati za kukopa na kutohoa msamiati unaotokana na Kiswahili na Kingereza.

Utafiti wa Owino (2003) ni tofauti na wetu katika misingi mbalimbali. Kwanza, utafiti wenyewe unashughulikia kipengee cha fonolojia ya maneno-mkopo (katika lugha ya Kijaluo). Maneno yenyewe ni yale yaliyokopwa/kutoholewa kutokana na Kingereza na Kiswahili. Kwa upande mwingine, utafiti wetu utajikita katika fonolojia na mofolojia ya msamiati wa Kijaluo (lahaja ya Nyanza Kusini) unaotokana na lugha ya Kiswahili.

Pili, utafiti wetu na ule wa Owino (2003) zinatofautiana katika mitazamo ya kinadharia. Kwa mfano, uchunguzi wa Owino (2003) uliongozwa na nadharia mbili: nadharia ya fonolojia vipande-sauti *(auto-segmental phonology)* ya Goldsmith (1967) na nadharia ya fonolojia ya konsonanti-vokali *(C-V phonology)* (Clement & Keyser, 1983). Kwa upande mwingine, utafiti wetu ulitekelezwa katika msingi wa Mkabala wa Mlingano Chanzi *(source similarity model)* kama ulivyoasisiwa na Smith (2009); mjadala wetu ulijikita katika mihimili ya nadharia hii. Kwa

hivyo, uchunguzi wetu ulichanganua fonolojia na mofolojia ya msamiati-mkopo katika lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini kwa mtazamo mpya uliojikita kwenye nadharia ya hivi karibuni.

Uchunguzi wa Owino (2003) ni muhimu kwetu kwani lugha zilizohusika ni miongoni mwa zile ambazo tulizifanyia uchunguzi (yaani Kijaluo na Kiswahili). Isitoshe, kipengele cha kiisimu alichoshughulikia cha fonolojia pia kitaangaziwa kwenye utafiti huu. Hii inamaana kuwa tutafaidika na mtazamo wake kuhusu vipengee vya fonolojia kama vile fonimu na silabi; vipashio ambavyo ni msingi wa utafiti wowote wa kifonolojia. Hata hivyo, utafiti huo una tofauti ya kipekee kwani umejikita katika nadharia mbili ambazo hazikutumika katika utafiti huu (ambazo ni nadharia ya Fonolojia Arudhi na nadharia ya Fonolijia ya Konsonanti-irabu). Hii ni tofauti na uchunguzi wetu ambao uliongozwa na Mkabala wa Mlingano Chanzi.

Pia, Oluoch, (2014) anachunguza maneno-mkopo katika lahaja ya Kijaluo ya Trans-Yala kutoka lugha jirani za Kiluhyia (lahaja za Kilumarachi na Kilunyala) na Kiswahili. Anaangazia mikakati ya kiutohozi inayopitiwa na maneno-mkopo kutoka lahaja za Kilumarachi, Kilunyala na Kiswahili kabla ya kuingizwa katika lahaja ya Kijaluo ya Trans-Yala. Utafiti huu unatekelezwa katika msingi wa Mkabala wa Mlingano Chanzi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wetu kwani unaangazia utohozi wa msamiati mkopo katika lahaja ya Kijaluo ya Trans-Yala na wakati huo huo unahusisha lahaja hiyo na lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini pamoja na lahaja za Kiluhyia (Kilumarachi na Kilunyala). Hali kama hii haifai kwani huibua mianya ya kuchanganya vipengele vya kileksimu katika lahaja zote mbili (za Kijaluo) zilizohusika. Dhana hii inatofautisha uchunguzi huu na wetu kwani utafiti wetu ulijikita katika lahaja moja pekee ya Kijaluo: lahaja ya Nyanza Kusini. Hii ilituwezesha kupata data ambazo zinahusiana moja kwa moja na lahaja ya Nyanza Kusini pekee.

Tofauti nyingine baina ya uchunguzi wa Oluoch (2014) na utafiti wetu ni kuwa Oluoch anashughulikia fonolojia na mofolojia ya maneno-mkopo yanayotokana na lugha ya Kiswahili na kuingizwa katika mfumo wa lahaja ya Kijaluo ya Trans-Yala huku utafiti wetu ukishughulikia fonolojia na mofolojia ya msamiati wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini uliokopwa kutoka lugha ya Kiswahili. Hili ni jambo muhimu kwani kuna tofauti bainifu za kimsamiati na kimatamshi baina ya lahaja hizi; tofauti ambazo zina uwezo wa kuathiri mkondo wa utohozi wa msamiati-mkopo.

Uchunguzi Oluoch (2014) utatufaa katika utafiti wetu kwa vile unahusu ukopaji wa msamiati katika Kijaluo kutokana na lugha za Kibantu (Lumarachi na Lunyala – ambazo ni lahaja za Kiluhya; na Kiswahili). Utafiti wetu pia unajihusisha na msamiati wa Kijaluo uliokopwa kutokana na Kiswahili – ambayo pia ni lugha ya Kibantu. Kwa hivyo, tunatarajia ulinganifu wa kiasi fulani katika mikakati itakayodhihirika kwenye harakati za kutohoa msamiati mkopo katika miktadha hii miwili ya kiuchunguzi.

Hali kadhalika utafiti wa Oluoch (2014) ulitumia mkabala ule ambao ndio utatumika katika uchunguzi wetu: Mkabala wa Mlingano Chanzi. Hii inaonyesha kuwa utafiti huu utakuwa ada kubwa kwa uchunguzi wetu. Hata hivyo, utafiti wa Oluoch (2014) unamulika zaidi msamiati – mkopo unaotokana na Kiluhyia (lahaja za Lumarachi na Lunyala), hivyo, kutopatia Kiswahili nafasi tosha katika utafiti wake. Hali kadhalika, uchunguzi huo uliangazia maneno-mkopo katika lahaja ya Kijaluo ya Boro-Ukwala na si lahaja ya Nyanza Kusini ambayo ndiyo itazingatiwa na utafiti huu.

## 1.9 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Mkabala wa Mlingano Chanzi ambao ni mtazamo kuhusu utohozi wa maneno-mkopo ulioasisiwa na Smith (2009). Mkabala wenyewe ulibuniwa kutokana na mihimili ya Nadharia ya Upeo (Prince & Smolensky, 1993).

### 1.9.1 Nadharia ya Upeo

Nadharia ya Upeo *(Optimality Theory)* (Prince & Smolensky, 1993) inajumlisha masharti bia ambayo yanatumiwa kuunda sarufi za lugha mahususi. Nadharia yenyewe ililenga kufafanua mchakato wa utohozi wa maneno-mkopo kwa kutumia muundo wa kifonolojia wa lugha pokezi pekee. Kwa mujibu wa Nadharia ya Upeo, maumbo ya lugha kama zinavyozungumzwa ni matokeo ya mtagusano baina ya kanuni zinazokinzana.

Maumbo ya nje ya lugha ni midhihiriko ya suluhu baina ya kanuni zinazokinzana na kushindana. Maumbo ya nje ndiyo 'upeo' kwani ndiyo yanayokiuka masharti yenye umuhimu mdogo zaidi kati ya masharti yote yanayoweza kukiukwa katika lugha maalum.

Nadharia ya Upeo inashikilia kuwa vipengele vya kiisimu ni vya aina mbili: vipengele tambulishwa na vipengele visivyotambulishwa. Vipengele visivyotambulishwa hupendelewa kwa vile ni bia kwani vinajitokeza katika sarufi zote. Vipengele tambulishwa navyo vinaepukwa na hutumiwa katika sarufi ili kuleta tofauti pekee. Mfano wa kipengele kisichotambulishwa cha muundo wa silabi ni kama vile: silabi zote ni wazi (kwani lugha nyingi huwa na silabi wazi – nazo lugha chache tu ndizo huruhusu silabi funge).

Awali, imetajwa kuwa Nadharia ya Upeo unaongozwa na kanuni maalum. Kanuni hizo ni za aina mbili: kanuni ya uaminifu na kanuni tambulishwa. Kanuni tambulishwa inasema kuwa umbo la neno lililotoholewa (neno-mkopo) litimize kanuni za umbo kama inavyoelekezwa na fonolojia

ya lugha pokezi. Kanuni ya uaminifu huelekeza kuwa neno-mkopo lidumishe sifa za umbo la kimsingi (linalotokana na lugha changizi), kwa hivyo kuleta ulinganifu wa aina fulani baina ya msamiati wa lugha changizi na ule wa lugha pokezi. Masharti ya uaminifu na masharti tambulishwa aghalabu hupingana. Umbo la lugha changizi hufanyiwa marekebisho yakiongozwa na masharti haya yaliyotajwa – ili kuunda msamiati-mkopo katika lugha-pokezi.

### 1.9.2 Mkabala wa Mlingano Chanzi

Kama ilivyotajwa hapo mbeleni, Mkabala wa Mlingano Chanzi (Smith, 2009) unatokana na mihimili ya Nadharia ya Upeo. Mkabala huu unaruhusu mikakati mbalimbali ya kiutohozi ambayo inatokana na uelewa (usio sahihi) wa mkopaji pamoja na fasiri za kifonolojia. Hali kadhalika, mkabala huu unasisitiza kanuni ya uaminifu baina ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo-tamkwa katika lugha pokezi. Kwa hivyo, kuna ulinganifu kati ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo la neno lililotoholewa.

Mahusiano ya lugha changizi na lugha pokezi yanahakikisha kuwa kuna kulingana baina ya umbo-tamkwa (la lugha pokezi) na umbo-fikirika (unaotokana na lugha changizi).Kwa hivyo, inasisitizwa kwamba vipengele vyote vya umbo la lugha changizi sharti vijitokeze katika umbo la lugha pokezi. Kwa upande wa pili, vipengele vyote katika umbo la neno katika lugha pokezi sharti vijitokeze katika umbo la neno la lugha changizi. Hata hivyo, Mkabala wa Mlingano Chanzi bado unaruhusu mikakati ya urekebishaji wa maneno-mkopo kwenye harakati za utohozi.

Umbo fikirika la lugha changizi unajengeka kutokana na ujuzi wa tahajia wa lugha hiyo, uelewa wa sarufi ya lugha changizi, pamoja na habari/fikra alizonazo mkopaji kuhusu lugha changizi. Umbo hili fikirika si lazima lifanane na umbo la neno linalotokana na lugha changizi (ambalo ndilo hutoholewa).

Umbo fikirika la msamiati wa lugha changizi hatimaye hufanyiwa marekebisho anuwai ili uweze kufuata masharti ya kifonolojia ya lugha pokezi. Kwa mfano, mkakati wa udondoshaji unaweza kutumiwa ili kuondoa vipande-sauti visivyo vya kimsingi.Hali kadhalika, Smith (2006) anadokeza kuwa uchopekaji aghalabu hutumiwa kurekebisha silabi zenye miundo isiyopendelewa. Zaidi ya hayo, mkabala huu wa Mlingano Chanzi hutambua kanuni zifuatazo za uaminifu:

*MAX – SB* ambayo huelekeza kuwa vipande-sauti vyote katika neno-changizi sharti vijitokeze katika neno lililotoholewa.

*DEP – SB* inasema kuwa vipande-sauti vyote katika msamiati-mkopo wa lugha pokezi sharti viwe katika lugha changizi. Hii ni kusema kwamba, kanuni hizi hazihimizi udondoshaji au uchopekaji.

Katika kutumia nadharia hii kwenye utafiti, mtafiti alilinganisha neno lililotoholewa na neno changizi ili kubainisha mikakati ya kiutohozi ambayo imezua leksimu ya lugha pokezi. Alibaini tofauti/ mfanano katika vipande-sauti vya leksimu za lugha changizi na zile za lugha pokezi. Hii ni kumaanisha kuwa mtafiti alikusudia kuweka wazi viwango vya kufikia/kutofikia kanuni za mkabala wa mlingano chanzi ambazo ni *MAX – SB* na *DEP – SB.* Hatimaye alitambua mikakati ya kiutohozi ambayo ilitumiwa katika kuzua leksimu katika lugha pokezi.

## 1.10 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii, tunaangazia vipengele viwili vya utafiti: ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data. Ukusanyaji wa data unahusu michakato yote itakayotumiwa na mfatiti ili aweze kupata msamiati wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini ambao umetoholewa kutoka lugha ya

Kiswahili. Kwenye uchanganuzi wa data, mtafiti anaonyesha jinsi alivyoyakabili maneno yaliyokopwa kwa nia ya kutimiza malengo ya utafiti.

### 1.10.1 Ukusanyaji Data

Data ambayo ilitumika katika utafiti huu ilijumuisha leksimu za Kiswahili ambazo zimeweza kuingia katika mfumo wa LKNK. Katika ukusanyaji wa data, mtafiti alipitia maandishi/machapisho mbalimbali yaliyoandikwa kwa LKNK . LKNK ndiyo inayotambuliwa kama lahaja sanifu ya Kijaluo kwa hivyo kutumika katika maandishi mengi ya Kijaluo (Owino, 2003). Kwa sababu hii, mtafiti aliteua machapisho mahususi ya Kijaluo ambayo kwayo aliweza kukusanya leksimu za Kijaluo zinazotokana na Kiswahili. Machapisho hayo ni: chapisho la Kijaluo la *Mano Doko Tim,* vitabu vya hadithi vya Kijaluo vya shule za msingi, Bililia ya Kijaluo pamoja na Kamusi ya Kijaluo.

Pia, mtafiti alitumia ujuzi wake wa lugha ya Kijaluo kuibua msamiati wa Kijaluo ambao unatokana na Kiswahili. Hali hii ilifanikishwa na dhana kwamba Kijaluo ndiyo lugha ya kwanza ya mtafiti na ameweza kukitumia kutoka utotoni. Isitoshe, mtafiti aliweza kutumia Kijaluo katika viwango vya awali vya shule za msingi. Ujuzi huu wa Kijaluo pia ulitumika pakubwa kwenye harakati za kutambua maneno ya Kijaluo yaliyokopwa kutokana na lugha ya Kiswahili kwani kuna tofauti bainifu kati ya leksimu asilia za lugha ya Kijaluo na zile zinazotokana na lugha ya Kiswahili hasa kwa kuzingatia miundo yao ya silabi. Ubainishaji huu wa msamiati uliokopwa ulithibitishwa na mzungumzaji mwingine asilia wa Kijaluo ambaye alisaidiana na mtafiti. Hali hii ilihakikisha kuwa kuna usahihi wa viwango vya juu katika utambuzi wa leksimu hizo. Hatimaye maneno hayo yalinukuliwa kiothografia na kisha kifonetiki.

Mtafiti alikusanya maneno themanini ya lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini ambayo yametoholewa kutokana na lugha ya Kiswahili. Maneno haya yalitokana na vikoa vifuatavyo vya

kisemantiki: uchukuzi, vifaa vya kinyumbani/jikoni, elimu, vyakula, mavazi, ukulima, afya, utawala, biashara, teknolojia ya mawasiliano, spoti na mazingira. Maneno hayo themanini ni yale ambayo yalithibitishwa kuwa yametoholewa kutokana na Kiswahili kwa kutumia umilisi wetu wa lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini

### 1.10.2 Utambuzi wa Maneno Mkopo

Owino (2003) anasema kuwa maneno mkopo huweza kutambuliwa kupitia utaratibu wa kulinganisha leksimu za lugha lengwa na zile za lugha changizi. Katika utafiti huu, ulinganishaji huu ulitegemea vigezo kama vile makaribiano ya kisemantiki kati ya dhana mbalimbali, mfanano wa kifonimu kati ya leksimu pamoja na mkondo wa ukopaji kati ya lugha husika. Kwa vile hakuna mahusiano kwenye asili za lugha hizi (Kiswahili na Kijaluo), pamoja na kuwepo kwa tofauti kubwa za kifonimu baina yao, haikuwa vigumu kubainisha msamiati wa Kijaluo uliotoholewa kutokana na Kiswahili. Hali kadhalika, Iribemwangi (2013) anatambua kuwa iwapo kuna ukopaji wa leksimu kutokana na mtagusano baina ya lugha, aghalabu pia kuna uwezekano wa kukopa vipengele vya kitamaduni vinavyohusishwa na lugha zenyewe. Yaani, iwapo msamiati wa Kijaluo utadhihirisha mfanano wa kimfumo na wa kidhana na ule wa Kiswahili, basi kuna uwezekano wa neno hilo kuwa la kimkopo. Harakati hizi zitaongozwa na ujuzi wa mtafiti wa lugha zinazotafitiwa.

### 1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kwa kutumia Mkabala wa Mlingano Chanzi ili kubainisha mikakati ya utohozi wa leksimu za Kiswahili zilizokopwa kutoka lugha ya Kijaluo. Katika mchakato huu, maneno ya Kijaluo yaliyokopwa kutoka Kiswahili yalibainishwa. Kisha, sauti zilizobadilishwa, zilizochopekwa na zilizodondoshwa kutambuliwa. Hali hii ndiyo ilimwezesha mtafiti kutambua mkakati wa utohozi uliotumika. Pia, maneno ya Kijaluo yaliyokopwa kutokana

na Kiswahili yalilinganishwa kifonolojia na maneno katika lugha changizi ili kubaini na kueleza kinadharia misingi ya ulinganifu/tofauti zilizokuwa baina ya lugha hizo mbili. Mchakato huo pia ulitekelezwa kwa kuzingatia vigezo vya kimofolojia.

Hatimaye matokeo ya uchanganuzi yaliwasilishwa kwa kutumia maelezo, mifano na vielelezo ambapo fonimu pamoja na silabi zinazobadilika zilionyeshwa huku mchakato husika wa kiutohozi ukitambuliwa. Baadhi ya michakato ya kiutohozi ambayo ilitarajiwa ni pamoja na uchopekaji, udondoshaji na ubadilishaji wa sifa za fonimu.

## 1.11 Hitimisho

Sura hii ya utangulizi imeonyesha masuala ya kimsingi katika uchunguzi huu. Imedhihirika kuwa utohozi wa maneno ya Kijaluo (kutokana na lugha ya Kiswahili) uliangaziwa katika viwango viwili vya kiisimu: fonolojia na mofolojia. Tathmini hii iliongozwa na Mkabala wa Mlingano Chanzi ambao unatokana na Nadharia ya Upeo. Mkabala huu unasisitiza mfanano wa kimaumbo wa vipande-sauti vya lugha husika: lugha changizi na lugha pokezi.

Katika sehemu inayofuata, tutadhihirisha fonolojia na mofolojia ya lugha zinazochunguzwa; yaani Kiswahili na Kijaluo. Hali hii itafanikisha uelewa wa namna vipande-sauti pamoja na maneno huingia katika Kijaluo kutoka Kiswahili kwenye utaratibu wa utohozi wa maneno.

# SURA YA PILI

# MISINGI YA KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA YA KIJALUO NA KISWAHILI

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii itaangazia vipengele vya kifonolojia na kimofolojia vya lugha zinazochunguzwa katika utafiti huu: Kijaluo na Kiswahili. Kuhusu fonolojia, tutabainisha konsonanti na irabu za Kijaluo na Kiswahili pamoja na miundo yake. Hali kadhalika, tutatambua fonimu za lugha ya Kijaluo na Kiswahili (konsonanti na irabu) na miundo ya silabi zao. Kuhusu mofolojia, tutaonyesha kimukhtasari vipengele vya kimsingi vya kimofolojia katika kila lugha (Kijaluo na Kiswahili). Misingi hii yote itatupatia mwelekeo unaofaa tutakapoanza kushughulikia michakato ya kiutohozi inayohusishwa na maneno ya Kijaluo yaliyokopwa kutokana na lugha ya Kiswahili.

## 2.2 Fonolojia za lugha Zinazotafitiwa

Fonolojia inafasiliwa kama tawi la isimu linalochunguza lugha mahususi kwa kuzingatia ruwaza ya sauti katika lugha yenyewe, miundo na ruwaza ya silabi pamoja na vipengele vya fonolojia kiarudhi. Kwa vile kila lugha ina mfumo wake wa kipekee, tutaanza kwa kushughulikia fonolojia ya Kijaluo na hatimaye fonolojia ya Kiswahili.

### 2.2.1 Fonolojia ya Kijaluo

Vigezo vya kifonolojia vitakavyoshughulikiwa hapa ni viwili: fonimu pamoja na silabi kwenye mukhtadha wa lugha ya Kijaluo. Lugha ya Kijaluo, kama lugha zingine, ina konsonanti, irabu pamoja na vipengele vya fonolojia arudhi. Konsonanti na irabu zikiwa ndizo zinazounda fonimu za Kijaluo; vigezo vyake vya kiarudhi vikiwa ni toni, mkazo pamoja na mchakato wa uwiano wa irabu (Okombo, 1982).

#### 2.2.1.1 Konsonanti za Kijaluo

Okombo (1982:17) anaeleza kwamba lugha ya Kijaluo ina konsonanti ishirini na moja (zikiwemo sauti mbili za nusu-irabu); pia ina sauti tano ambazo ni vizuiwa-nazali ambatano. Kwa jumla, Kijaluo kina fonimu ishirini na sita za konsonanti. Jedwali lifuatalo linaonyesha konsonanti za Kijaluo:

**Kielelezo 2: Konsonanti za Kijaluo**

| **Hati ya Kiothografia** | **Hati ya Kifonetiki** | **Mfano wa Neno** | **Maana (kwa Kiswahili)** |
|---|---|---|---|
| p | p | /pur/ | ukulima |
| b | b | /bul/ | ngoma |
| w | w | /witʃ/ | kichwa |
| m | m | /matʃ/ | moto |
| f | f | /fuwɔ/ | ujinga |
| th | θ | /θɔ/ | kifo |
| dh | ð | /ðiaŋ/ | ng'ombe |
| t | t | /ɔt/ | nyumba |
| d | d | /djɛl/ | mbuzi |
| r | r | /ridɔ/ | kaza |
| l | l | /lilɔ/ | kuchafua |
| s | s | /san/ | sahani |
| n | n | /nɔnɔ/ | sufuri |
| ch | tʃ/č | /tʃak/ | maziwa |
| j | ɟ/ǰ | /ɟi/ | watu |
| y | j | /jiɛn/ | mti |
| ny | ɲ | /ɲarɔja/ | ndama |
| k | k | /kiɲ/ | kesho |
| g | g | /gini/ | kitu hiki |
| ng' | ŋ | /ŋija/ | uniangalie |

| Hati ya Kiothografia | Hati ya Kifonetiki | Mfano wa Neno | Maana (kwa Kiswahili) |
|---|---|---|---|
| h | h | /hɔnɔ/ | muujiza |
| mb | mb | /mbaka/ | gumzo |
| ndh | nð | /anðɔga/ | msaliti |
| nd | nd | /ndalɔ/ | siku |
| nj | ɲɟ | /ɲɟugu/ | njugu |
| ng | ŋg | /ŋgɔrɔ/ | mwoga |

Fonimu ambazo Okombo (1982) anarejelea kama vizuiwa-nazali ambatano ni /mb/, /nð/, /nd/, /ɲɟ/ na /ŋg/. Hata hivyo, mtazamo wetu ni kuwa si sahihi kuita sauti hizi vizuiwa-nazali ambatano *(nasal-stop compounds)* kwa vile baadhi yao hazina kiungo cha kizuiwa. Mfano ni /nð/ ambayo inaundwa kutokana na nazali na kikwamiza. Kuita sauti hizi vizuiwa-nazali ambatano inapotosha kwa sababu hiyo ni sawa na kusema kuwa kila moja ina kiungo cha nazali na kizuiwa; hali ambayo haijitokezi katika sauti /nð/. Kwingineko, Adhiambo (1981) naye anajumuisha sauti hizi pamoja na nazali. Maoni yetu ni kuwa, kuna maana zaidi katika kurejelea sauti hizi kama nazali-ambatano ili kuonyesha kuwa zinaundwa kutokana na kuambatishwa kwa sauti kadhaa, moja wapo ikiwa ni nazali. Hii ndiyo istilahi ambayo tumetumia kurejelea sauti hizi katika kazi hii.Konsonanti za Kijaluo zimepangwa kimukhtasari katika jedwali lifuatalo kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: jinsi ya kutamka, mahali pa kutamkia pamoja na hali ya ughuna.

**Kielelezo 3: Jedwali la Uinisho wa Konsonanti za Kijaluo**

| Mahali pa Kutamkia / Namna ya Kutamka | Midomo | Midomo na Meno | Meno | Ufizi | Kaakaa Gumu | Midomo na Kaakaa Laini | Kaakaa Laini | Koromeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuiwa | p<br>b | | | t<br>d | č<br>ɟ | | k<br>g | |
| Vikwamizwa | | f<br>v | θ<br>ð | s | | | | h |
| Kitambaza | | | | l | | | | |
| Kimadende | | | | r | | | | |
| Viyeyusho | | | | | j | w | | |
| Nazali | m | | | n | ɲ | | ŋ | |
| Nazali Ambatani | mb | | nð | nd | ɲǰ | | ŋg | |

Jedwali limetokana na Okombo (1982:19) na Oduor (2002:73).

Katika jedwali hili (kwenye safu inayobainisha namna ya kutamkia), konsonanti sighuna zimewekwa kwenye eneo la juu nazo zile ghuna ziko katika eneo la chini.

Okombo (1982) anaeleza kuwa obstruenti za kaakaa gumu katika Kijaluo (/č/ na /ɟ/) ambazo zinaonyeshwa kwenye jedwali kama vizuiwa kwa uhakika si vizuiwa wala vizuiwa-kwamizwa; zinapatikana katikati ya makundi haya mawili.Hivyo, zinaweza kuingizwa katika kundi lolote kati ya makundi haya mawili; yaani kundi la vizuiwa au lile la vizuiwa-kwamizwa.

#### 2.2.1.2 Irabu za Kijaluo

Maoni ya wataalamu yanatofautiana katika ubainishaji wa irabu za Kijaluo. Kwa mfano, Okombo (1982) anashikilia kuwa Kijaluo kina irabu tisa; msimamo ambao ndio unaochukuliwa na Oduor (2002). Hata hivyo, waandishi kama vile Tucker (1974) wanasema kuwa Kijaluo ni lugha yenye fonimu kumi za irabu. Katika mjadala huu, mtazamo wetu ni kuwa Kiluo kina irabu kumi; msimamo unaochukuliwa na wataalamu wengi.

Kwa mujibu wa Okombo (1982:19-20), 'Irabu za Kijaluo hutokea katika jozi nne, kila jozi ikiwa na irabu mbili; moja ikiwa na sifa ya mzizi wa ulimi ulio mbele *(+ATR)* na nyingine ikiwa na mzizi wa ulimi ulio nyuma *(–ART)'*.Hali kadhalika, kuna irabu moja ambayo inajisimamia. Katika utamkaji wa irabu yenye sifa ya mzizi wa ulimi ulio mbele, ulimi huskumwa mbele na kusababisha mwanya mkubwa zaidi kwenye koromeo. Kwingineko, irabu zenye sifa ya mzizi wa ulimi ulio nyuma zinapotamkwa, mzizi wa ulimi huvutwa nyuma. Irabu zenyewe ni kama zifuatazo:

**Kielelezo 4: Unukuzi wa Irabu wa Kijaluo Kiothografia/Kifonetiki**

| Unukuzi Kiothografia | Uwasilishaji Kifonetiki |
|---|---|
| A, a | a |
| E, e | e, ɛ |
| I, i | I, i |
| O, o | o, ɔ |
| U, u | u, ʊ |

Jedwali hili ni kwa mujibu wa Okombo (1982).

Ni dhahiri kwamba, hati ya kiothografia haidhihirishi tofauti katika sifa ya mzizi wa ulimi baina ya irabu mbalimbali za Kijaluo. Lifuatalo ni jedwali la irabu za Kijaluo linaloonyesha sifa za kimsingi za irabu zenyewe: sehemu ya ulimi na mwinuko wa ulimi.

**Kielelezo 5: Jedwali la Uainisho wa Irabu za Kijaluo**

| **Sehemu ya Ulimi** / **Mwinuko wa Ulimi** | Mbele | Kati | Nyuma |
|---|---|---|---|
| Juu | i | | u |
| Kati Juu | I | | ʊ |
| Kati | e | | o |
| Kati Chini | ε | | ɔ |
| Chini | | a | |

Jedwali limetokana na Oduor (2002:76).

Zaidi ni kwamba, irabu za Kijaluo pia zinaweza kupambanuliwa kwa msingi wa umbo la mdomo ambapo tunapata makundi mawili ya irabu hizo: irabu za mdomo ulioviringwa na zile za mdomo uliotandazwa. Irabu za mdomo uliotandazwa ni zile za mbele na kati (/i/, /I/, /ε/, /e/, /a/) nazo irabu zote za nyuma hutamkwa kwa mdomo ulioviringwa (/u/, /ʊ/, /o/, /ɔ/).


### 2.2.1.3 Silabi za Kijaluo

Uelewa wa silabi za lugha ni dhana msingi katika ufafanuzi wa fonolojia ya lugha hiyo. Oduor (2002:47-50) anapoeleza maana ya silabi, ananukuu mwana-isimu Gimson (1989) anayetoa fasili ya silabi kama kiungo ambacho ni kubwa zaidi kuliko fonimu (kipande-sauti) na kinachobainika kutokana na neno au mofimu. Katika mchakato wa kufafanua kwa undani zaidi dhana ya silabi, Oduor anatoa mielekeo ya wataalamu mbalimbali kuhusu silabi.

Mwanzo, Oduor (2002) anatambua mwelekeo wa kimapokeo ambao umejengeka katika sintaksia. Anamnukuu Goldsmith (1990) anayesema kwamba silabi ni kiambajengo kinachoweza kufasiliwa katika muktadha wa miundo virai; hali inayotokea katika sentensi pia. Ufafanuzi wake unatambua vijisehemu anuwai vya silabi: mwanzo *(onset),* kilele *(peak/nucleus)* na kifungio *(coda).* Kilele na kifungio kwa pamoja hurejelewa kama kina cha silabi *(core/rhyme).* Hii ni kumaanisha kuwa silabi imegawanywa katika sehemu mbili kuu: mwanzo na kina. Viungo hivi vinaweza kufupishwa kwa njia ifuatayo (Njogu na wengine, 2006:18).

| **Neno** | **Kifupisho** |
|---|---|
| Silabi | SI |
| Mwanzo | MW |
| Kina | KI |
| Kilele | LE |
| Kifungio | FU |

Kwa mfano, katika neno la Kijaluo *kom* (kiti), muundo wa ndani wa silabi ya neno hili $kɔm$ huweza kuonyeshwa katika mchoro ufuatao:




Mchoro huu unadhihirisha mtazamo wa fonolojia ya konsonanti-vokali kuhusu muundo wa silabi. Ngala (1994: 9) anaarifu kuwa silabi ya Kijaluo huweza kuwa na irabu moja pekee; hii ndiyo kilele na ni sehemu ya lazima katika silabi ya Kijaluo. Pia, anatambua kuwa silabi ya Kijaluo ina konsonanti isiyozidi moja katika sehemu ya mwanzo; hali ni vivyo hivyo katika sehemu ya kina cha silabi.

### 2.2.1.4 Miundo ya Silabi za Kijaluo

Lugha ya Kijaluo ina miundo ya silabi wazi na silabi funge (Oduor, 2002). Silabi wazi huishia kwa sauti ya irabu nayo silabi funge huishia kwa sauti ya konsonanti. Aina hizi za silabi pia huweza kufasiliwa katika muktadha wa kuwepo/kutokuwepo kwa kifungio ambapo Njogu na wengine (2006) wanasema kuwa silabi wazi hazina kifungio nazo silabi funge zina konsonanti kama kifungio/kimalizio chake. Huu ni mtazamo wa fonolojia ya konsonanti-vokali.

Oduor (2002:81) anabainisha sura mbalimbali za silabi wazi katika Kijaluo na kuziweka kwenye makundi anayobandika herufi A hadi E. Pia, anabainisha sura anuwai za silabi funge na kuziweka kwenye makundi anayobandika herufi F hadi J.

**(i) Aina A (Muundo wa KI)**

Silabi ya aina A imeundwa kutokana na konsonanti ikifuatana na irabu.

| | | |
|---|---|---|
| a. bɛti | panga | KI $ KI |
| b. rɛmɔ | damu | KI $ KI |
| c. maðɔ | kunywa | KI $ KI |

**(ii) Aina B (Muundo wa I)**

Silabi ya aina B imeundwa kutokana na irabu moja ya wakaa mfupi pekee; haina mwanzo.

| | | |
|---|---|---|
| a. ibirɔ | 'umekuja' | I $ KI $ KI |

**(iii) Aina C (Muundo wa KI :)**

Hii ni silabi yenye sauti ya konsonanti moja ikifuatwa na irabu moja yenye wakaa mrefu.

| | | |
|---|---|---|
| a. θo: | kuchoshwa na mambo | KI: |
| b. θɔ | umande | KI: |

**(iv) Aina D (Muundo wa I :)**

Silabi ya muundo huu huwa imejengwa kutokana na irabu moja yenye wakaa mrefu.

| | | |
|---|---|---|
| a. e: | ndiyo | I: |
| b. i: | kupigana | I: |

**(v) Aina E (Muundo wa KII)**

Katika aina hii ya silabi, konsonanti moja hufuatwa na irabu mbili mfululizo; aghalabu irabu zenyewe huwa ni za juu.

| | | |
|---|---|---|
| a. fuɔlɔ | kikohozi | KKI $ KI |
| b. θuɔlɔ | nafasi | KII $ KI |

**(vi) Aina F (Muundo wa KIK)**

Huu ni muundo mmoja wa silabi funge katika Kijaluo.

| | | |
|---|---|---|
| a. mit | tamu | KIK |
| b. matʃ | moto | KIK |
| c. gin | wao | KIK |

**(vii) Aina G (Muundo wa IK)**

Katika silabi ya muundo huu, irabu moja ya wakaa mfupi hufuatwa na sauti ya konsonanti.

| | | |
|---|---|---|
| a. ɔt | nyumba | IK |
| b. un | nyinyi | IK |
| c. an | mimi | IK |

**(viii) Aina H (Muundo wa KI: K)**

Silabi hii huanza kwa sauti ya konsonanti inayofuatwa na irabu ya wakaa mrefu na kumalizika kwa konsonanti.

| | | |
|---|---|---|
| a. ǰo:w | nyati | KI:K |

**(ix) Aina I (Muundo wa I: K)**

Muundo huu wa silabi huwa na irabu moja ya wakaa mrefu inayofuatwa na sauti ya konsonanti.

**(x) Aina J (Muundo wa KIIK)**

Huu ni muundo wa silabi ya Kijaluo wenye konsonanti moja inayofuatwa na irabu mbili (mfululizo) za juu halafu mwishowe ni konsonanti.

| | | |
|---|---|---|
| b. duog | rudi | KIIK |
| c. guok | mbwa | KIIK |

Ingawa Oduor (2002) anasema kuwa Kijaluo kina silabi yenye muundo wa KI: K (aina H), ni maoni yetu kuwa hakuna silabi yenye muundo huu katika katika lugha ya Kijaluo (hasa lahaja ya Nyanza Kusini). Kwamba, mfano unaotumiwa na Oduor (2002) kuonyesha muundo huu wa silabi haudhihirishi matamshi kamili ya neno lenyewe kwa mujibu wa lahaja ya Nyanza Kusini. Neno hilo ni [jo: wi] na si [jo:w] kama anavyodai Oduor (2002). Hivyo, muundo kamili wa silabi za neno hilo ni KI: $KI. Hii ni kumaanisha kuwa, neno hilo lina silabi mbili wala si moja. Silabi ya kwanza ikiwa na muundo wa KI: nayo ya pili muundo wake ukiwa ni KI. Kwa uhakika, wazo letu ni kuwa, lahaja ya Kijaluo ya Nyanza Kusini haina naneno yenye muundo huo wa silabi (KI:$K).

### 2.2.2 Fonolojia ya Kiswahili

Vigezo vya kifonolojia vya Kiswahili vimejengeka katika msingi kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu; hivyo, kuna mfanano mkubwa kifonolojia baina ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Hali kadhalika, kuna vipengele ambavyo vimetokana na harakati za ukopaji wa msamiati kutoka lugha zingine. Harakati hizi zimeingiza mifumo geni katika lugha ya Kiswahili. Lugha ambazo zimeathiri Kiswahili kwa namna hii ni pamoja na Kiarabu, Kijerumani, Kireno, Kingereza, miongoni mwa lugha zingine. Kwa mfano, Mwaliwa (2014) anatambua vipande-sauti ambavyo vimeingia katika lugha ya Kiswahili kutoka Kiarabu kupitia ukopaji wa maneno. Miongoni mwao ni fonimu /ð/, /θ/ na /ɣ/; hatimaye sauti hizi zimekuwa sehemu ya fonolojia ya Kiswahili. Njogu na wengine (2006:10) wanatambua sauti zifuatazo kama fonimu za Kiswahili:

**Kielelezo 6: Jedwali la Fonimu za Kiswahili**

| Othografia | Unukuzi Kifonetiki | Mfano wa Neno |
|---|---|---|
| a | a | apa |
| e | ɛ | ɛnda |
| i | i | ita |
| o | ɔ | ɔa |
| u | u | ua |
| p | p | papa |
| t | t | tia |
| k | k | kua |
| ch | ʧ/č | ʧapa |
| b | b | bɛba |
| d | d | dua |
| ng' | ŋ | ŋɔa |
| f | f | fua |
| j | ɟ/ǰ | ǰua |
| g | g | gari |
| m | m | miwa |
| n | n | nɔa |
| ny | ɲ | ɲama |
| mb | mb | amba |
| nd | nd | ndɔ : |
| nj | ɲǰ | ɲǰɔ : |
| ng | ŋg | ŋguvu |
| th | θ | θamani |
| s | s | sɛma |
| sh | ʃ | ʃɔmbɔ |
| h | h | hɔfu |
| v | v | va : |
| dh | ð | fɛða |
| z | z | zua |
| r | r | rara |
| l | l | lima |
| y | j | jaja |
| gh | ɣ | ɣala |
| w | w | wɛmbɛ |

#### 2.2.2.1 Konsonanti za Kiswahili

Wataalamu wametoa maoni yanayohitilafiana kuhusu idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili. Kwa mfano, Mgullu (1999) anadokeza kuwa Kiswahili kina konsonanti ishirini na nne (bila kujumuisha nusu-irabu mbili). Kwa upande mwingine, Njogu na wengine (2006) wanadai kuwa lugha ya Kiswahili ina idadi ya konsonanti ishirini na tisa. Hali kadhalika, Mweri (2010) naye anashikilia kuwa idadi ya konsonanti za Kiswahili ni thelathini na tatu naye Mwaliwa (2014) anabainisha konsonanti ishirini na tano za Kiswahili.

Kubainisha idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili ni swala la kimsingi katika utafiti huu. Sababu ni kuwa, fonimu hizi ndizo kiini cha utohozi wowote unaohusisha lugha ya Kiswahili.Kwa hivyo, sharti tutathmini fikra mbalimbali za wataalamu ambao wamewahi kuzungumzia mada hii kabla ya kuchukua msimamo kuhusu swala hili tata.

Tofauti zinazoibuka miongoni mwa wataalamu kuhusu idadi ya konsonanti za Kiswahili zinatokana mambo kadhaa.Kwanza ni kutambuliwa/kutotambuliwa kwa nazali-ambatani kama fonimu mahususi zinazojisimamia katika lugha ya Kiswahili. Nazali-ambatani ni pamoja na /mb/, /nd/, /ŋg/, /ɲǰ/, /nz/ na nyinginezo. Kwa mfano, Njogu na wengine (2006) na Mweri (2010) wanaibuka na idadi zao za konsonanti kutokana na kujumuisha nazali-ambatani zote za Kiswahili katika orodha za fonimu za konsonanti. Mgullu (1999) na Mwaliwa (2004) nao hawatambui nazali-ambatani katika orodha hiyo ya konsonanti za Kiswahili. Swali tunalojiuliza ni iwapo nazali-ambatani ni fonimu zinazojisimamia au la. Nazali-ambatani ni sauti-mwambatano ambazo zina uwezo wa kutekeleza majukumu sawa na fonimu zingine za lugha husika. Hata hivyo, nazali-ambatani huundwa kutokana na fonimu tofauti za Kiswahili zinazotamkwa pamoja; moja baada ya nyingine. Lakini hii si sababu tosha ya kuingiza sauti hizi kwenye kundi la fonimu za lugha husika. Kimukhtasari, mtazamo wetu ni kuwa, nazali-ambatani

hazina nafasi kama mojawapo ya fonimu za Kiswahili. Badala yake, vipashio hivi ni msururu wa fonimu zenye uamilifu ulio sawa na fonimu za Kiswahili.

Pia, fikra tofauti za wataalamu kuhusu idadi ya konsonanti za Kiswahili hutokana na nafasi za fonimu Kiswahili zenye asili ya kigeni. Kwa mfano, Mwaliwa (2014) anazua mjadala kuhusu nafasi ya sauti [x] katika fonolojia ya Kiswahili. Mtazamo wake ni kuwa, sauti hii si fonimu ya Kiswahili kwa vile haina uwezo wa kutofautisha maana katika maneno ya Kiswahili (hata yale yaliyokopwa kutoka Kiarabu). Badala yake, inabainisha maana katika maneno ya Kiarabu (ambayo ndiyo asili yake) pekee.

Katika mjadala huu unaohusu sauti [x], fikra yetu ni kuwa, maoni ya Mwaliwa (2014) yana mashiko zaidi. Sababu ni kwamba, fonimu inastahili kuwa na uwezo wa kubainisha maana katika maneno. Hivyo, kipashio kisichoweza kutimiza masharti hayo hakiwezi kuwa fonimu. Kwa vile Mwaliwa (2014) anaonyesha kuwa sauti [x] haina uwezo wa kutofautisha maana katika maneno ya Kiswahili, basi sauti hii si fonimu ya Kiswahili. Matarajio yetu ni kuwa, iwapo ingekuwa fonimu ya Kiswahili, basi ingekuwa na uwezo wa kutofautisha maana hasa katika maneno-mkopo ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Utata unaotokana na msimamo huu hata hivyo ni kubainisha nafasi ya sauti hii [x] katika fonolojia nzima ya Kiswahili. Ni dhahiri kuwa, kipande-sauti hiki kinatumika katika baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo yamekopwa kutokana na lugha za kigeni (hasa Kiarabu). Katika hali kama hii, hatujui namna ya kukirejelea kipande-sauti hiki katika muktadha wa fonolojia ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni maoni yetu kuwa swala hili linastahili kutathminiwa zaidi kupitia uchunguzi wa kina.

Lifuatalo ni jedwali la fonimu za konsonanti za Kiswahili:

**Kielelezo 7: Jedwali la Uainisho wa Konsonanti za Kiswahili**

| **Mahali pa Kutamkia** / **Aina** | Midomo | Midomo na Meno | Meno | Ufizi | Kaakaa Gumu | Kaakaa Laini | Glota | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vikwamizwa | | f<br>v | θ<br>ð | s<br>z | ʃ | ɣ | h | 9 |
| Vizuiwa | p<br>b | | | t<br>d | | k<br>g | | 6 |
| Nazali | m | | | n | ɲ | ŋ | | 4 |
| Vizuiwa kwamizwa | | | | | ʧ<br>ǰ | | | 2 |
| Kitambaza | | | | l | | | | 1 |
| Kimadende | | | | r | | | | 1 |
| Viyeyusho | w | | | | j | | | 2 |
| | | | | | | | | Konsonanti 25 |

Jedwali hili limetokana na Mgullu (1999: 69) likiwa na nyongeza/mabadiliko machache.

Mabadiliko yaliyotekelezwa katika jedwali la Mgullu (1999) ni kama yafuatayo: viyeyusho vimeingizwa kwenye jedwali lenyewe; konsonanti /ʃ/ iliainishwa kama sauti inayotamkwa katika meno na ufizi (bali si kaakaa gumu), hali ambayo inapotosha. Konsonanti hii ni kikwamizwa ambacho kinatamkwa katika kaakaa gumu bali si katika meno na ufizi.Mwisho, tumeondoa kikwamizwa-ghuna cha kaakaa laini [x] kwenye jedwali (kwa mujibu ya ufafanuzi uliotolewa hapo awali). Hali hii inatupatia jumla ya konsonanti ishirini na tano. Sauti hizi ndizo zitakuwa uti wa mgongo wa utohozi wa sauti za Kiswahili za konsonanti zinazoingia katika Kijaluo.

#### 2.2.2.2 Irabu za Kiswahili

Idadi ya sauti za irabu za Kiswahili haina utata mwingi kama ilivyo konsonanti. Kutokana na utafiti wetu, wataalamu wengi wa lugha ya Kiswahili wanakubaliana kuwa kuna fonimu tano za irabu katika lugha ya Kiswahili. Wataalamu hawa ni pamoja na Mgullu (1999), Ngoju na wengine (2006), Mweri (2010) miongoni mwa wengine. Fonimu hizo ni /i/, /ɛ/, /a/, /ɔ/ na /u/.

Fonimu hizi zinabainishwa katika msingi wa vigezo vitatu vikuu: mahali pa kutamkia (sehemu ya ulimi), mwinuko wa ulimi na mkao/umbo la mdomo. Kwa kuzingatia misingi hii, irabu hizi huainishwa kwa njia ifuatayo (Mgullu, 1999):

**(i) Mahali pa kutamkia:**

1.) Irabu za mbele /i/ na /ɛ/

2.) Irabu za nyuma /u/ na /ɔ/

3.) Irabu ya kati /a/

**(ii) Mwinuko wa ulimi :**

4.) Irabu za juu ni /i/ na /u/

5.) Hakuna irabu za nusujuu

6.) Irabu ya chini ni /a/


**(iii) Mkao wa midomo :**

8.) Irabu za mdomo mviringo ni /u/ na /ɔ/

9.) Irabu za mdomo mtandazo ni /i/ na /ɛ/

Uainishaji huu unaweza kuonyeshwa kwenye mchoro ufuatao:

**Kielelezo 8: Mchoro wa Uainisho wa Fonimu za Irabu**




Mchoro umetokana na Mgullu (1999).

### 2.2.2.3 Silabi za Kiswahili

Maoni anuwai yametolewa na wataalamu kuhusiana na silabi za Kiswahili. Kwa mfano, Clement & Keyser, (1983) anaponukuliwa na Owino (2003:79) wanadai kuwa Kiswahili huainishwa kama lugha ya aina ya pili (II) kwa kuzingatia muundo wake wa silabi. Hii ni kwa mujibu wa Clement & Keyser, (1983) anaponukuliwa na Owino (2003:79). Lugha ya aina hii (aina II), inaruhusu miundo miwili ya silabi: muundo wa irabu moja pekee (I) na muundo wa konsonanti na irabu (KI).

Kwingineko, Njogu na wengine (2006:17) wanasema: 'silabi asilia ya Kiswahili ni wazi yaani hazina kifungio, daima huwa na irabu ya mwisho ambayo vilevile hujenga kilele cha silabi hiyo'. Isitoshe, wanaongezea kwamba lugha ya Kiswahili pia huweza kuwa na silabi funge hasa inapokopa maneno kutokana na lugha zenye silabi funge.Hata hivyo, lugha ya Kiswahili haina silabi funge kiasilia.

### 2.2.2.4 Miundo ya Silabi za Kiswahili

Mgullu (1999:73) anabainisha miundo saba ya silabi za Kiswahili. Miundo hiyo ni kama ifuatayo:

**(i) Silabi za Konsonanti + Irabu (K+I)**

Muundo wa KI ndio unaopendelewa zaidi katika lugha ya Kiswahili; unatumika zaidi kuliko miundo mingine yote. Muundo huu unaweza kuonekana katika maneno yafuatayo:

a. darasa      da$ra$sa

b. mifano      mi$fa$nɔ

**(ii) Silabi za Irabu (I)**

Silabi za irabu pekee huwa na irabu moja ambayo inajisimamia kama silabi.

a. ua      u$a      I

b. pia      pi$a      I

**(iii) Silabi za Konsonanti (K)**

Konsonanti ambazo zina uwezo wa kuwa silabi katika lugha ya Kiswahili ni zile za aina ya nazali pekee. Konsonanti za nazali ni pamoja na /m/, /n/, /ɲ/ na /ŋ/. Mifano ya silabi zenye muundo huu ni kama vile :

a. mti      m$ti

b. mke      m$kɛ

Mgullu (1999) anashikilia kuwa nazali zenye uwezo wa kujisimamia kama silabi ni mbili tu: /m/ na /n/. Anatumia vielelezo vifutavyo kudhihirisha hali hii:

a. mpaka      m$pa$ka

b. mtu      m$tu

c. alipiga a$li$m$pi$ga

d. nchi n$tʃi

e. nta n$ta

Isitoshe, Mwita (2009) naye anadokeza kwamba nazali zinazoweza kuchukua nafasi ya kilele cha silabi katika lugha ya Kiswahili ni /m/ na /n/. Pamoja na mifano mingine, anatumia neno 'nchi' kuonyesha hali hii ambapo anabainisha silabi za neno hili (kama n$tʃi).

Hata hivyo, mtazamo huu huenda una dosari kwani kuna mifano inayoonyesha kuwa nazali zote huweza kujisimamia kama silabi katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili. Hali hii inadhihirika katika maneno yafuatayo (yametokana na Njogu na wengine, 2006) :

a. nchi ɲ$tʃi

b. nge ŋ$ŋgɛ

c. ngwe ŋ$ŋgwɛ

Katika mjadala huu, mtazamo wetu ni kwamba, fikra za Mgullu (1999) pamoja na wataalamu wengine zinatokana na kuchanganya hati za kiothografia na hati za kifonetiki. Hali hii ndiyo inayoleta utata katika silabi ya mwanzo kwenye maneno kama vile 'nchi' na 'ncha' ambapo kiothografia silabi ya kwanza ni 'n' ilhali katika uwasilishaji kifonetiki ni 'ɲ'. Kwa hivyo, umbo ambalo tunazingatia ni ule unaotokana na matamshi (umbo la kifonetiki) ambalo ni 'ɲ'. Hitimisho yetu ni kuwa, nazali zote za Kiswahili huweza kujisimamia kama silabi katika baadhi ya maneno ya Kiswahili.

**(iv) Silabi Konsonanti+Konsonanti + Irabu (KKI)**

Kwenye muundo wa KKI, konsonanti mbili hufuatana na irabu moja. Hata hivyo, si konsonanti zote huweza kushiriki katika mfuatano kama huu. Konsonanti ambazo huweza kuchukua sehemu

ya mwanzo ya silabi ni za aina tatu: nazali (/m/ na /n/); vizuiwa (/p/, /t/, /k/, /b/, /d/ na /g/) na vizuiwa-kwamizwa (/ɟ/ na /tʃ/). Hali hii inadhihirika katika mifano ifuatayo :

a. omba ɔ$mba I$KKI

b. enda ɛ$nda I$KKI

c. ngao ŋga$ɔ KKI$I

d. chwiwa ʧwi$wa KKI$½ II

**(v) Silabi za Konsonanti + Nusu-irabu + Irabu (K ½ II)**

Silabi ya K ½ II inaundwa kutokana na sauti ya konsonanti inayofuatwa na sauti moja ya nusu-irabu na mwishowe irabu. Silabi hizi aghalabu huwa na fonimu za konsonanti mbalimbali, nusu-irabu na irabu za kila aina. Mifano ni kama ifuatayo:

a. mwezi mwɛ$zi K ½ II$KI

b. pweza pwɛ$za K ½ II$KI

c. bwawa bwa$wa K ½ II$ ½ II

d. vyangu vja$ŋgu K½II$KKI

**(vi) Konsonanti + Konsonanti + Nusu-irabu + irabu (KK ½ II)**

Muundo huu wa konsonanti mbili zinazofuatwa na nusu-irabu na kisha irabu unajitokeza katika maneno machache tu ya Kiswahili.

a. ngwara ŋgwa$ra KK ½ II $KI

b. ngwenje ŋgwɛ$ɲǰɛ KK ½ II $KKI

**(vii) Silabi Funge**

Silabi funge ni silabi ambazo huishia kwa sauti ya konsonanti. Wataalamu wamebainisha kuwa lugha ya Kiswahili ina mfumo wa silabi wazi. Mwita (2009) anasisitiza wazo hili kwa kuwanukuu Polome (1967), Myachina (1991) pamoja na Mohammed (2001). Ingawa maneno

yanayokopwa kutokana na lugha zingine hutoholewa ili yaweze kufuata mifumo ya lugha pokezi, wakati mwingine miundo geni ya kifonolojia huweza kudumishwa katika lugha pokezi. Mwita (2009) anatambua jambo hili anaposema kuwa kuingizwa kwa maneno-mkopo katika lugha ya Kiswahili kumepanua upeo wa miundo ya silabi za lugha ya Kiswahili. Hali kama hiyo ndiyo inayoibua mifumo ya silabi funge katika lugha ya Kiswahili. Njogu na wengine (2006:21) wanatoa maoni yafuatayo kuhusu silabi funge za Kiswahili:

> Maneno yanayokopwa na kuingizwa katika Kiswahili hujaribu kutoholewa ili yaafikiane na muundo asili wa Kiswahili. Hata hivyo, kuna baadhi ya maneno-mkopo ambayo yamezidi kuhifadhi baadhi ya sifa zake asilia hata baada ya kuingia katika lugha ya Kiswahili.

Njogu na wengine (2006) wanapiga hatua na kutambua maumbo manne ya silabi ambayo yameingia katika lugha ya Kiswahili kwa njia hii. Maumbo hayo ni: KIK, KKKI, IK, na KKIK. Katika orodha hii, kuna umbo moja tu ambao si wa silabi funge (muundo wa KKKI); miundo yote iliyobaki ni ya silabi funge. Ifuatayo ni mifano ya maneno ya Kiswahili yenye miundo ya silabi funge zilizobainishwa (Njogu na wengine, 2006):

**(i) Silabi ya KIK**

a. maktaba mak$ta$ba

b. bakshishi bak$ʃi$ʃi

c. leksia lɛk$si$a

d. muktadha muk$ta$ða

**(ii) Silabi ya KKIK**

a. spekta spek$ta

b. trakta trak$ta

**(iii) Silabi ya IK**

a. oksijeni ok$si$ɟ$ɛni

Maneno ya Kiswahili yenye silabi funge yamekopwa kutokana na lugha kama vile Kingereza, Kiarabu, Kijerumani, na nyinginezo. Mgullu (1999) kwa upande wake anaorodhesha maneno yafuatayo kama mifano ya silabi funge katika lugha ya Kiswahili :

| | | |
|---|---|---|
| b. alhamisi | al$ha$mi$si | IK$KI$KI$KI |
| c. ilhali | il$ha$li | IK$KI$KI |
| d. daftari | daf$ta$ri | KIK$KI$KI |
| e. labda | lab$da | KIK$KI |
| f. inkshafi | ink$ʃa$fi | IKK$KI$KI |

## 2.3 Mofolojia za Lugha Zinazotafitiwa

Mofolojia ni tawi la isimu ambalo hushughulikia uambishaji pamoja na mifumo ya mofimu katika lugha mahususi. Kwenye sehemu hii, tutajadili jinsi viambishi tofautitofauti huambatishwa katika mizizi ya nomino za lugha hizi (Kiswahili na Kijaluo) ili kudhihirisha hali mbalimbali za nomino hizo. Kwanza tutaangazia mofolojia ya nomino za Kijaluo ikifuatwa na mofolojia ya Kiswahili.

### 2.3.1 Mofolojia ya Nomino za Kijaluo

Mofolojia ya nomino za Kijaluo itajikita katika mofimu ambazo zinaambatishwa katika mizizi ya nomino za Kijaluo ili kutoa maaana mbalimbali za nomino zenyewe. Hivyo, sehemu hii itashughulikia mofimu zinazowakilisha hali ya uwingi na hali za umilikaji *(genitive)* katika nomino za Kijaluo.

#### 2.3.1.1 Uwingi wa Nomino katika Kijaluo

Okombo (1982:29) anatambua njia nne ambazo hutumiwa kuunda nomino za wingi katika Kijaluo:

i. Udondoshaji wa irabu ya mwisho katika nomino za umoja.

ii. Uchopekaji wa viambiship-tamati vya uwingi kwenye mzizi (baada ya kudondoa irabu ya mwisho katika nomino). Aghalabu viambishi hivi ni {i} na {e}.

iii. Ubadilishaji wa konsonanti ya mwisho katika mzizi wa neno.

iv. Urekebishaji *(readjustment)* wa sifa za irabu kwa mujibu wa kanuni za uwiano.

Hali hizi zinajitokeza katika vielezo viifuatavyo:

(a) Nomino zinazopata uwingi kwa kupachikwa kiambishi tamati kwenye mizizi yao:

| Umoja | Wingi | Maana (Kiswahili) |
|---|---|---|
| a. bandɔ | bɛnd**ni** | hindi/mahindi |
| b. agwata | agwɛt**ni** | kibuyu/vibuyu |

Kiambishi cha wingi kilichoambatishwa kwenye nomino hizi ni {ni}.

(b) Nomino zinazopata uwingi kwa kudondoshwa kwa irabu zao mwisho:

| Umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|
| a. gwɛn**ɔ** | gwɛn | kuku/kuku |
| b. wuɔʧ**e** | wuɔʧ | kiatu/viatu |

Irabu zilizoandikwa kwa herufi zilizokolea ndizo zinadondoshwa ili kupata umbo la wingi.

(c) Nomino zinazopata uwingi kwa kubadilishwa kwa konsonanti ya mwisho kwenye mizizi ya nomino zenyewe:

| Umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|
| a. ɔndiɛ**k** | ɔndiɛ**gi** | fisi/fisi |
| b. rua**θ** | ruɛ**ð**i | fahali/mafahali |
| c. pwɔ**ð**ɔ | pwɔ**θ**ɛ | shamba/mashamba |

Kwa jumla, uwingi wa nomino katika Kijaluo unaweza kuonyeshwa kwa kudondoa irabu ya mwisho katika neno linalorejelea umoja ama kwa kupachika mofimu ya wingi (kama kiambishi tamati) katika mzizi wake. Baadhi ya mofimu zenye maana ya uwingi ni kama vile {ni} na {i}. Hali kadhalika, konsonanti ya mwisho kwenye mzizi/shina la neno huweza kubadilishwa kwa namna mbalimbali ili kuwasilisha dhana ya wingi.

### 2.3.1.2 Hali za Umilikaji katika Nomino za Kijaluo

Hali ya umilikaji *(genitive)* ni umbo la nomino ambalo huwasilisha mahusiano ya nomino hiyo na maneno mengine. Okombo (1982:32) anasema kuwa katika lugha ya Kijaluo, nomino ambayo humilikiwa ndiyo inayofanyiwa mabadiliko yanayoonyesha mhusika mmiliki *(genitive case).* Hii ni kweli kwani mofimu inayobainisha mhusika mmiliki hupachikwa kwenye nomino inayomilikiwa. Hali hii inaonekana katika mifano ifuatayo:

| Nomino | | Hali ya Umiliki | Maana |
|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | | |
| a. gwɛnɔ | gwɛn | gwɛnd | kuku wa |
| b. ɔmɛna | ɔmɛndɛ | ɔmɛnd | dagaa wa |
| c. ðiaŋ | ðɔk | ðiaŋg | ng'ombe wa |

d. guɔk guɔgi guɔg mbwa wa

Kwa hivyo, kuna mifanyiko miwili mikuu ambayo inahusishwa na uundaji wa maumbo ya hali za umilkaji katika lugha ya Kijaluo. Kwanza ni udondoshaji wa irabu ya mwisho (iwapo irabu hiyo ipo katika neno husika). Pili ni ubadilishaji wa konsonanti ya mwisho kwenye shina la neno.

### 2.3.2 Mofolojia ya Nomino za Kiswahili

Kama ilivyo katika lugha zingine za Kibantu, nomino za Kiswahili huwekwa katika makundi (ngeli) kwa kuzingatia vigezo vya kifonolojiia, kimofolojia na kisintaksia. Katika sehemu hii, tutazingatia kigezo cha kimofolojia kwani ndicho kinachohusiana na eneo letu la utafiti.

Wataalamu mbalimbali wa isimu wameainisha ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia na kuibua makundi tofauti tofauti ya nomino zenyewe. Miongoni mwao ni Waihiga (1999) anayetambua ngeli nane za nomino za Kiswahili ambazo zinatokana na viambishi awali vya nomino hizo. Mgullu (1999:52) naye anabainisha ngeli tisa za nomino za Kiswahili huku wakiweka ngeli hizi katika makundi manne:

**i.** Ngeli sita za nomino zilizo na viambishi awali vyote viwili (vya umoja na wingi).

**ii.** Ngeli moja ya nomino zilizo na kiambishi cha umoja tu pamoja na mofu kapa ya wingi.

**iii.** Ngeli moja ya nomino zilizo na kiambishi awali cha wingi tu pamoja na mofu kapa ya umoja.

**iv.** Ngeli moja ya momino zisizo na kiambishi awali popote.

Kwingineko, Mbaabu (1988:40) anaainisha ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia kwa kutumia nambari.Kwake, nambari hizi ndizo zinazotumiwa kutambulisha ngeli mbalimbali za nomino. Kwa jumla, zifuatazo ni mukhtasari wa ngeli za kimofolojia za Kiswahili:

**Kielelezo 9: Jedwali la Ngeli za Kimofolojia za Kiswahili**

| Nambari | Viambishi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|
| 1-2 | M-WA | msomi | wasomi |
| 3-4 | M-MI | maji | maji |
| 5-6 | JI-MA | jina | majina |
| 7-8 | KI-VI | kichwa | vichwa |
| 9-10 | N-N | njia | njia |
| 11-10 | U-N | uso | nyuso |
| 12/13/14 | PA/KU/MU | mahali (hapa/huku/mle) | mahali (hapa/huku/mle) |

Jedwali limetokana na Njogu na wengine (2006).

Kuna ngeli ya KA-TU (12-13) ambayo inajitokeza katika jedwali la Njogu na wengine (2006). Hata hivyo, ni maoni yetu kuwa Kiswahili sanifu hakina ngeli kama hii kwa vile ni nadra kimatumizi kukumbana na tungo zenye nomino zilizo na viambishi awali vinavyobainishwa na ngeli hii. Kwa sababu hiyo, hatujajumuisha ngeli hiyo katika jedwali letu la ngeli za kimofolojia za Kiswahili. Hali hii inatupa jumla ya ngeli 15 na si 17 kama ilivyobainishwa na Njogu na wengine (2006).

Uainishaji wa nomino za Kiswahili katika ngeli hizi za kimofolojia ni tofauti na hali ilivyo katika mfumo wa lugha ya Kijaluo kwa vile Kiswahili ni lugha ya Kibantu nayo Kijaluo ni lugha ya

Kiniloti. Nomino za Kijaluo hazina makundi yanayotokana na viambishi awali vya nomino zenyewe. Sifa hiyo haipatikani katika lugha ya Kijaluo.

Makundi haya ya nomino za Kiswahili yana umuhimu wa kipekee kwenye uchanganuzi wa utohozi wa kimofolojia kwani yatafanikisha uelewa wa namna ambavyo nomino zenye viambishi awali mbalimbali hutoholewa kabla ya kuingizwa katika mfumo wa Kijaluo. Isitoshe, swala la namna ambavyo lugha-pokezi (Kijaluo) itakavyokabili mifumo ya viambishi awali vya nomino za Kiswahili ni kipengele ambacho kina umuhimu. Uchanganuzi huu utafanywa huku tukizingatia kuwa Kijaluo hakina mfumo wa viambishi awali katika nomino zake. Badala yake, mofu nyingi katika nomino hujikeza kama viambishi tamati. Hivyo basi, nafasi za viambishi awali katika baadhi ya nomino za Kiswahili utohozi unapotokea ni kipengele muhimu.

## 2.4 Hitimisho

Sura ya pili imeshughulikia maumbo ya lugha zinazohusika katika utafiti huu kwenye misingi ya kifonolojia. Maumbo ya vipande-sauti vya kila lugha yameonyeshwa waziwazi kuanzia fonimu hadi silabi. Tathmini ya vigezo hivi vya kifonolojia zinaonyesha kuwa baadhi ya vyambajengo vya lugha hizi mbili vinafanana kifonetiki. Hata hivyo, pia kuna vipande-sauti ambavyo ni mahususi katika kila lugha.

Kutokana na hali hizi, tunatarajia kuona mkondo utakaochukuliwa na vipande-sauti vinavyopatikana katika lugha zote mbili kwenye utaratibu wa utohozi. Hali kadhalika, tunatarajia kuona namna ambavyo vipande-sauti visivyopatikana kwenye lugha-pokezi (Kijaluo) ilhali viko katika lugha-changizi (Kiswahili), hukabiliwa kwenye mchakato mzima wa utohozi wa maneno ambayo yana vipashio vya aina hii.

# SURA YA TATU

# UTOHOZI WA KIFONOLOJIA

## 3.1 Utangulizi

Katika sehemu hii, tutaangazia michakato ambayo Kijaluo hutumia inapotohoa leksimu kutoka lugha ya Kiswahili ili leksimu kama hizo ziweze kuchukua mifumo ya kifonolojia ya Kijaluo. Katika harakati hizo, tutashughulikia utohozi wa fonimu zinazotokana na Kiswahili pamoja na mikakati yake na pia utohozi wa silabi zinazoingia katika Kijaluo kutoka Kiswahili.

Hali kadhalika, tutalinganisha neno changizi na neno pokezi kifonolojia huku tukifafanua sababu za kuwepo kwa mfanano au tofauti baina ya pande hizo mbili. Uchanganuzi huu utaongozwa na mtazamo wa mlingano chanzi kwa mujibu wa Smith (2009). Mtazamo wa mlingango chanzi unasizitiza mfanano kati ya umbo fikirika wa neno changizi na umbo la msamiati mkopo. Mkabala huu unautazama utohozi kama mchakato wenye pande mbili: upande wa kinachoingia na upande wa tokeo. Upande wa kinachoingia una msamiati wa lugha changizi nao upande wa tokeo una msamiati uliohotewa.

## 3.2 Utohozi wa Fonimu

Kiswahili na Kijaluo hutofautiana katika msingi wa fonimu zinazopatikana katika kila lugha. Hii ni kusema kwamba kuna konsonanti zinazopatikana katika lugha moja na si ile nyingine. Kwa sababu hii, leksimu ya lugha pokezi inapoundwa kutokana na fonimu zisizopatikana katika lugha changizi, lugha-pokezi inalazimishwa kutohoa fonimu za aina hiyo ili zikubalike kwenye mfumo wa lugha pokezi.

Fonimu za lugha changizi zisizopatikana katika lugha pokezi huweza kugeuzwa na kuwa ile inayokaribiana nayo katika mfumo wa lugha pokezi. Kwa hivyo, tunatarajia kuwa fonimu za

Kiswahili ambazo hazipatikani katika Kijaluo zitageuzwa na kuwa zile zenye sifa za karibu kifonolojia katika upande wa Kijaluo.

Pia, umbo katika upande wa kinachoiingia ni umbo fikirika la neno changizi bali si umbo la ndani la neno lenyewe (la lugha changizi). Katika utaratibu mzima wa utohozi, vipande sauti visivyo muhimu (kwenye fikra) huweza kudondoshwa.

### 3.2.1 Utohozi wa Irabu

Kuna tofauti katika idadi ya irabu za Kijaluo na zile za Kiswahili. Kwa mfano, ilibainishwa hapo awali (2.2.2) kuwa irabu za Kijaluo zinajitokeza katika jozi; kila jozi likiwa na irabu mbili; hali kadhalika, kuna irabu moja zaidi inayojisimamia. Hii inamaanisha kuwa Kijaluo kina jumla ya irabu tisa (Okombo, 1982). Hii ni tofauti na Kiswahili ambacho kina irabu tano: /i/, /ε/, /a/, /ɔ/ na /u/ (Mgullu, 1999; Njogu na wengine, 2006; Mweri, 2010; Iribemwangi, 2010). Kutokana na tofauti hizi, tunatarajia kuwa irabu tano za Kiswahili zitaweza kuingia katika mfumo wa irabu tisa za Kijaluo utohozi unapofanyika. Pia, imebainika kuwa irabu zote tano za Kiswahili zinapatikana katika lugha ya Kijaluo (Owino, 2003).

Uchunguzi wetu unaonyesha kwamba katika leksimu nyingi za Kijaluo zinazotokana na Kiswahili, fonimu za irabu zinadumishwa bila kufanyiwa mabadiliko yoyote. Ifuatayo ni mifano inayodhihirisha hali hii:

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. kalεnda | kalεnda |
| b. ǰikɔni | ǰikɔn |
| c. mzabibu | musabibu |
| d. gɔdɔrɔ | gɔðrɔ |

Mifano hii inaonyesha kuwa irabu zote za Kiswahili zinaweza kudumishwa katika lugha ya Kijaluo utohozi unapotokea. Kwa mujibu wa kanuni za mkabala wa mlingano chanzi, vipande sauti vyote katika neno-changizi sharti vijitokeze katika neno-mkopo. Isitoshe, vipande-sauti vyote katika neno-mkopo sharti viwe katika neno-pokezi. Inajitokeza katika mifano iliyotolewa kwamba irabu zote za Kiswahili zinajitokeza kwenye mfumo wa Kijaluo bila mageuzi yoyote. Hii ni kusema kwamba, utohozi wa fonimu za irabu kutoka Kiswahili unazingatia kanuni za mkabala wa mlingano chanzi (kanuni ya uaminifu).

Hata hivyo, uchunguzi wetu unaonyesha kuwa kuna baadhi ya irabu ambazo zinabadilika katika mchakato wa utohozi. Hali hii inajitokeza katika mifano ifuatayo:

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. tarɛhɛ | tar**i**k |
| b. bɛndɛra | b**a**ndɛra |
| c. mkɔŋgɛ | makɔŋg**a** |
| d. s**u**ruru | s**a**ruru |

Mifano hii inaonyesha kuwa kuna mabadiliko ya irabu yanayoweza kutokea katika utohozi wa irabu za Kijaluo kutoka Kiswahili. Hata hivyo, ni muhimu kubainisha kuwa mabadiliko kama haya hutokea kwa nadra. Mabadiliko hayo ni kama yafuatayo:

a. /ɛ/ > [a]/ [i]

b. /i/ > [ɛ]

c. /ɔ/ > [a]

d. /u/ > [a]

Kama ilivyotajwa hapo awali, mabadiliko kama haya ni nadra kwani yanatokea katika maneno machache tu kwenye harakati ya utohozi. Kwa hivyo, si rahisi kutambua mazingira ya kutokea kwao. Kwa sababu hii, si rahisi kuibua sheria zinazobainisha mazingira ya mageuzi ya aina hii.

Ingawa mabadiliko haya yanaonekana kuenda kinyume na kanuni ya uaminifu (ya mkabala wa mlingano-chanzi) inayoelekeza kuwa vipande-sauti vilivyomo kwenye neno-mkopo viwe katika neno changizi, imebainika kuwa irabu katika neno-mkopo ina mahusiano ya kifonolojia na irabu katika neno changizi. Kwenye mifano yetu, irabu ya mbele kati tandaze /ɛ/ hugeuka na kuwa ya mbele juu tandaze [i]; irabu hizi mbili zinakaribiana kifonolojia kwani zote ni irabu za mbele tandaze. Hali kama hiyo ndiyo inayojitokeza irabu /i/ inapogeuka na kuwa [ɛ]. Hali kadhalika, irabu ya nyuma kati mviringe /ɔ/ inageuka na kuwa irabu ya kati-chini tandaze /a/. Irabu hizi mbili zinapakana kifonolojia: moja ni ya kati na nyingine ni ya chini.

Hali hii inadhihirisha kwamba utohozi unapofanyika, irabu ya neno-mkopo hujaribu kukaribiana kadri inavyowezekana na ile ya neno-changizi. Hii inamaanisha kuwa mchakato wa utohozi unajaribu kudumisha ulinganifu kati ya vipande-sauti vya neno-changizi na neno-mkopo kwa mujibu wa masharti ya mkabala wa mlingano chanzi. Hata hivyo, irabu ya nyuma juu viringe /u/ inapobadilika na kuwa irabu ya kati chini tandaze [a] (kwa mfano: /sururu/ kuwa [saruru]) ni hali isiyoelezeka katika mkabala wa mlingano chanzi. Sababu ni kwamba, katika mfano huu, mchakato wa utohozi unazidisha tofauti baina ya vipande-sauti vya neno-changizi na vile vya neno-mkopo. Hii ni kinyume na mhimili wa mkabala wa mlingano chanzi unaohimiza uaminifu kati ya vipande sauti vya lugha changizi na vile vya lugha pokezi. Kwa hivyo, kichocheo cha hali kama hii hakielezeki katika mkabala wa mlingano chanzi.

### 3.2.2 Utohozi wa Konsonanti

Hapo awali, tulibainisha konsonanti za Kiswahili na zile na Kijaluo. Ilijitokeza kwamba Kijaluo kina idadi ya konsonanti ishirini na sita (Okombo, 1982) sawa na Kiswahili ambayo pia ina konsonanti ishirini na sita. Hata hivyo, kuna sauti za konsonanti katika lugha ya Kiswahili ambazo hazipatikani katika lugha ya Kijaluo. Konsonanti hizo ni: /ʃ/, /ɤ/, /z/, na /v/. Konsonanti nyingi za Kiswahili ambazo pia hupatikana katika Kijaluo aghalabu hudumishwa msamiati unapokopwa nazo zile za Kiswahili zisizopatikana katika Kijaluo hugeuzwa kifonetiki.

#### 3.2.2.1 Udumishaji wa Konsonanti

Konsonanti nyingi za Kiswahili pia hupatikana katika lugha ya Kijaluo.Utafiti wetu unaonyesha kuwa konsonanti hizi aghalabu hudumishwa katika leksimu zinazotoholewa. Konsonanti zinazopatikana katika lugha hizi mbili ni kama zifuatazo:

a. Vikwamizwa: /f/, /v/, /θ/, /ð/, /s/, /h/

b. Vizuiwa: /b/, /t/, /d/, /k/, /g/

c. Nazali: /m/, /n/, /ɲ/, /ŋ/

d. Vizuiwa-kwamizwa: /ǰ/, /ʧ/

e. Kitambaza: /l/

f. Kimadende: /r/

g. Viyeyusho: /w/, /j/

Baadhi ya nazali-ambatani zinazopatikana katika Kiswahili pia ziko katika lugha ya Kijaluo; nazali hizo ni: /mb/, nd/, /ɲǰ/ na /ŋg/. Yafuatayo ni maneno ya Kijaluo ambayo yamedumisha konsonanti za Kiswahili kwenye msamiati uliokopwa (kwa mujibu wa uchanguzi wetu):

| Kiswahili | Kijaluo |
| --- | --- |
| a. ʧupa | ʧupa |
| b. mananasi | mananas |
| c. mkɔngɛ | makɔŋga |
| d. ndimu | ndim |

Kanuni ya kijumla inayoongoza udumishaji wa konsonanti ni kuwa konsonanti zote za Kiswahili zinazopatikana katika Kijaluo hudumishwa katika maneno ya Kijaluo kwenye utaratibu wa utohozi. Hata hivyo, kuna hali chache zinazoonyenyesha mabadiliko ya konsonanti; hali hizi zitaangaziwa mbeleni. Mifano hii inadhihirisha ya kwamba, utohozi wa sauti za konsonanti unazingatia kwa kiwango kikubwa kanuni ya uaminifu – kama inavyopendekwa kwenye mkabala wa mlingano chanzi. Maumbo yanayojitokeza katika lugha changizi (Kiswahili) yanatokea moja kwa moja katika lugha pokezi (Kijaluo).Wakati huo huo, maumbo ya lugha pokezi pia yakuwepo kwenye lugha changizi. Kwenye muktadha huu, maumbo haya yanawakilishwa na fonimu za konsonanti katika msamiati unaotoholewa.

Ingawa konsonanti nyingi za Kiswahili zimedumishwa katika maneno yaliyokopwa kuingia Kijaluo, ni kweli kwamba kuna baadhi ya konsonanti ambazo zinageuka katika mchakato huu wa ukopaji wa maneno. Hali hii inatokea licha ya kwamba sauti hizo za konsonanti zinapatikana katika mifumo ya lugha zote mbili.

Uchanganuzi wetu umeonyesha kuwa zifuatazo ni sauti zinazogeuka katika baadhi ya maneno utohozi unapofanyika (ingawa konsonanti zenyewe zimo katika lugha changizi na lugha pokezi):

**/b/ > [mb]**

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. buibui | mbui |
| b. kirɔbɔtɔ | ɔmbɔtɔ |

**/l/ > [r]**

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. filimbi | firimbi |
| b. matɔfali | matafarɛ |
| c. rɛli | rɛru |

**/d/ > [ð]**

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. gɔdɔrɔ | gɔðrɔ |

**/l/ > [t]**

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. ʧampali | ʧampat |

**/r/ > [l]**

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. risasi | lisasi |

Katika mabadiliko haya, ni vigumu kuibua kanuni inayozingatiwa kwa vile mabadiliko kama haya yanatokea kwa nadra na katika maneno machache pekee. Hata hivyo, vielelezo hivi vinaonyesha kuwa kuna tofauti kati ya umbo la lugha changizi na ule wa lugha pokezi: hali

inayotishia kukiuka kanuni ya uaminifu ya mkabala wa mlingano chanzi. Hata hivyo, masharti ya uaminifu yanasisitiza ulinganifu wa umbo tamkwa la lugha pokezi na umbo fikirika la lugha changizi. Umbo fikirika la lugha changizi unaibuka kutokana na uelewa wa mzungumzaji kuhusu lugha changizi. Uelewa huu huweza kuwa sahihi au usio sahihi. Vipengele vinavyochangia uelewa huu ni pamoja na ujuzi wa tahajia wa lugha yenyewe, uelewa wa sarufi yake na fikra za msemanji kuhusu lugha changizi. Kwa mujibu wa mhimili huu wa mkabala wa mlingano chanzi, ni mtazamo wetu kuwa kubadilishwa kwa konsonanti zinazopakina katika lugha pokezi ni kutokana na fasiri isiyosahihi ya konsonanti husika katika lugha changizi. Kwa mfano fonimu /b/ (kipasuo sighuna cha mdomoni ya Kiswahili katika neno kama vile 'bata') inafasiriwa visivyo na msemaji wa Kiluo kama nazali ambatani [mb] hivyo kuibua neno *'mbata'*, katika Kijaluo baada ya utohozi. Hali hii ndiyo inayoibua mageuzi mengine kama vile /l/ kuwa [r]; /d/ kuwa [ð] pamoja na mifano mingine iliyoonyeshwa hapo awali.

### 3.2.2.2 Ubadilishaji wa Konsonanti

Konsonanti zinazobadilika wakati wa utohozi aghalabu huwa ni zile zilizomo katika lugha changizi ingawa hazipatikani katika lugha pokezi. Kwenye utafiti wetu, sauti hizi ni zile ambazo zimo katika Kiswahili na kusosekana katika Kijaluo. Ilibainishwa kuwa konsonanti hizo ni nne: /ʃ/, /ɤ/, /z/ na /v/.

Antilla (1972) anasema kuwa kwenye harakati za kukopa leksimu, mzungumzaji hutambua sifa bainifu za sauti geni na kuzigeuza na kuwa zile zinazokaribiana nazo zaidi katika mfumo wa lugha pokezi. Hivyo basi, tunatarajia kuwa maneno yanapotoholewa, konsonanti hizi tano zitabadilishwa katika lugha ya Kijaluo na kuwa zile ambazo zina sifa za karibu za kifonetiki–kati ya fonimu zile za Kijaluo.

Uchanganuzi wetu unadhihirisha kuwa kikwamwizwa sighuna cha kaakaa gumu /ʃ/ na kikwamizwa ghuna cha ufisi /z/ zote hubadilishwa na kuwa kikwamizwa hafifu cha ufizi [s] katika lugha ya Kijaluo. Zaidi ni kwamba, kikwamizwa ghuna cha mdomo-meno /v/ hubadilika na kuwa kipasuo ghuna cha mdomo [b] nayo kikwamizo ghuna cha kaakaa laini /ɣ/ hugeuka na kuwa kipasuo ghuna cha kaakaa laini [g]. Hali hizi zinadhihirika katika maneno yafuatayo:

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
|---|---|
| a. ʃemeǰi | semeǰi |
| b. nazi | nas |
| c. ɣasia | gasia |
| d. ʧumvi | ʧumbi |

Kwa kutumia sifa bainifu za kimatamshi za fonimu, tunaweza kuonyesha sheria zinazoelekeza mabadiliko haya kwa namna zifuatazo:

**(a) /ʃ/ > /s/**

$$\begin{bmatrix} +\text{Kons} \\ +\text{Kikw} \\ -\text{Ghuna} \\ +\text{Kaakaa gumu} \\ +\text{Kif} \end{bmatrix} > \begin{bmatrix} +\text{Ufizi} \end{bmatrix} \Big/ \text{Kiswahili}$$

**(b) /z/ > /s/**

[+ Kons
+ Kikw
+ Ufizi
+ Kif
+ Ghuna] > [-Ghuna] / Kiswahili

**(c) /ɣ/ > /g/**

[+ Kons
+ Kikw
+ Ghuna
+ Kaakaa laini
+ Kif] > [+ kipasuo] / Kiswahili

**(d) /v/ > /b/**

[+ Kons
+ Kikw
+ Ghuna
+ Midomo-meno
+ Kif] > [+ Midomo] / Kiswahili

Mabadiliko haya ya kisauti yanaweza kufafanuliwa ipasavyo kwa kutumia mtazamo wa mlingano chanzi. Hapo awali, ilidokezwa kwamba mtazamo huu unasisitiza mfanano baina ya umbo katika lugha-changizi na ule wa lugha-pokezi. Hata hivyo, umbo unaorejelewa wa lugha

changizi ni umbo kama unavyofikiriwa na msemaji wa lugha inayokopa msamiati. Umbo hili si lazima ufanane na ule wa ndani wa lugha changizi kwani huenda umbo hili una makosa. Msingi wake ni ujuzi wa mzungumzaji wa lugha changizi, ujuzi ambao unaweza kuwa na upungufu.

Hali ambayo inajitokeza hapa ni kwamba, sauti za Kiswahili zisizopatikana katika Kijaluo zinafasiriwa visivyo (na mzungumzaji wa Kijaluo) na kubandikwa zile zinazokaribiana nazo. Kwa hivyo, mageuzi hayo ni matokeo ya fasiri zisizosahihi za sauti za Kiswahili. Hii ndiyo maana sauti hizi katika lugha ya Kijaluo zina mahusianao ya kimatamshi na zile za lugha changizi (Kiswahili) kwa mfano /ʃ/ inapobadilika na kuwa [s], mahusiano baina ya sauti hizi ni kuwa zote ni vikwamizwa ambazo ni ghuna. Hivyo basi [s] ya Kijaluo imetokana na fasiri isiyosahihi ya fonimu ya Kiswahili /ʃ/ katika harakati za ukopaji wa msamiati. Mtazamo huo wa mkabala wa mlingano chanzi ndio ambao unatupa yale mabadiliko mengine yanayotokea tunapotohoa leksimu za Kiswahili zenye sauti zisizopatikana katika Kijaluo. Mabadiliko ni: /ɣ/ kuwa [k] (kiwamizwa ghuna cha kaakaa laini kupewa umbo la kikwamizwa sighuna cha kaakaa laini); /z/ kuwa [s] (kikwamizwa ghuna cha ufizi kupewa umbo la kikwamizwa sighuna cha ufizi); /v/ kuwa [b] (kikwamizwa ghuna cha mdomo-meno kupewa umbo la kipasuo ghuna cha mdomo) miongoni mwa mageuko mengine. Kwa jumla, inadhihirika kwamba katika fikra za mkopaji, mfanano unadumishwa baina ya sauti za lugha ya Kijaluo na ile ya Kiswahili; hali hii inasisitizwa na kanuni ya mkabala wa mlingano chanzi.

Hali hizi zina misingi yao katika kanuni za mkabala wa mlingano chanzi. Kanuni zenyewe ni mbili: vipande-sauti vyote katika neno-changizi viwe katika neno-pokezi *(MAX – SB)* na vipande-sauti vyote katika neno-mkopo viwe katika neno-changizi *(DEP – SB)*. Kwa hivyo, mahusiano ya karibu kati ya kipashio cha lugha changizi na kile cha lugha pokezi yanatokana na

nia ya kudumisha ulinganifu katika vipande-sauti vya lugha mbili zinazohusika kwenye mchakato wa utohozi.

### 3.3 Utohozi wa Silabi

Katika sura ya pili, ilibainika kuwa kuna tofauti bainifu kwenye miundo ya silabi za Kijaluo na zile za Kiswahili. Ilijitokeza kuwa lugha ya Kiswahili ina muundo wa silabi wazi nayo Kijaluo ina silabi wazi na funge. Katika harakati za utohozi wa maneno kutoka lugha ya Kiswahili, miundo ya silabi huweza kubadilika. Kwa mfano, silabi wazi ya Kiswahili inaweza kubadilika na kuwa silabi funge katika Kijaluo. Ili muundo wa silabi funge/wazi uweze kupatikana katika lugha ya Kijaluo, kuna michakato mbalimbali ya kifonolojia inayotumiwa kwenye harakati za kutohoa maneno ya Kiswahili. Michakato hiyo imejadiliwa katika sehemu inayofuata.

#### 3.3.1 Mifanyiko Inayohusishwa na Utohozi wa Silabi

Kijaluo hutumia michakato anuwai katika harakati za kutohoa silabi za Kiswahili ili kupata maneno yanayofuata kanuni za kifonolojia za Kijaluo. Kwa vile lugha hizi zote (Kijaluo na Kiswahili) hukubali mifumo ya silabi wazi, mara nyingi mikakati mingi hulenga kuibua silabi funge katika maneno yanayokopwa kutokana na Kiswahili. Kwingineko, michakato hii pia husaidia kutohoa silabi za Kiswahili zinazoundwa na nazali moja pekee kwani sauti za nazali moja haina usilabi katika Kijaluo. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu, mifanyiko inayohusishwa na utohozi wa silabi ni udondoshaji, ubadili na uchopekaji.

##### 3.3.1.1 Udondoshaji

Njogu na wengine (2006: 27) wanatoa fasili ya udondoshaji kama 'hali ambapo kipashio cha neno (irabu, konsonanti au silabi) hutoweka katika mazingira maalum'. Hii ni kusema kuwa udondoshaji unaweza kuathiri fonimu au silabi.

Uchanganuzi umeonyesha kuwa utohozi wa leksimu zinazotokana na Kiswahili unajumuisha udondoshaji wa fonimu na udondoshaji wa silabi. Kwa mujibu wa mkabala wa mlingano chanzi, vipande sauti ambavyo hudondoshwa ni vile visivyo vya kimsingi katika fonolojia ya lugha husika (lugha pokezi).Katika muktadha wa utafiti huu, vipande sauti vitakavyodondoshwa utohozi unapofanyika ni vile visivyo na umuhimu katika lugha ya Kijaluo. Data zetu zinadhihirisha viwango viwili vya udondoshaji:

a) Udondoshaji wa fonimu

b) Udondoshaji wa silabi

**a) Udondoshaji wa Fonimu**

Uchunguzi umedhihirisha kuwa undondoshaji wa fonimu unaweza kujitokeza kwa namna mbili: udondoshaji-kati na udondoshaji-mwisho. Udondoshaji-kati ni kutoweka kwa sauti katikati ya neno ilhali udondoshaji-mwisho ni kutoweka kwa sauti mwishoni mwa neno. Mifano ya udondoshaji-kati kwenye utohozi wa leksimu za Kijaluo zinazotokana na Kiswahili ni kama ifuatayo:

| Kiswahili | Kijaluo |
|---|---|
| a. sɛr**i**kali | sirkal |
| b. ma**f**uta | mauta |
| c. gɔd**ɔ**rɔ | gɔðrɔ |
| d. t**w**iga | tiga |

Katika mifano hii, sauti za Kiswahili zilizoandikwa kwa herufi nzito zinadondoshwa kwenye mchakato wa utohozi; hii ndiyo maana sauti hizi haziko katika safu ya maneno ya Kijaluo.

Inajitokeza hapa kwamba, udondoshaji-kati unaweza kuathiri sauti za irabu, nusu-irabu au konsonanti.

Kwingineko, udondoshaji-mwisho unatokea sauti iliyo mwishoni mwa neno inapoondolewa kwenye harakati ya utohozi. Hali hii inadhihirika katika maneno yafuatayo:

| Kiswahili | Kijaluo |
|---|---|
| a. kaput**i** | kabut |
| b. mʃip**i** | masip |
| c. ŋgum**i** | aŋgum |
| d. wakil**i** | ɔkil |

Maneno haya yanaonyesha kuwa irabu ya mbele juu tandaze /i/ katika maneno ya Kiswahili (irabu ya mwisho katika kila neno) imedondoshwa. Huu ndio udondoshaji-mwisho. Udondoshaji-mwisho aghalabu ndio ambao hugeuza silabi wazi za Kiswahili na kuunda silabi funge katika Kijaluo. Kwa jumla, udondoshaji-mwisho wa fonimu hutokea mara nyingi kuliko undondoshaji-kati wakati wa utohozi. Kanuni ya udondoshaji-mwisho ni kuwa irabu inadondoshwa inapochukua nafasi ya kilele katika silabi wazi inayojitokeza mwishoni mwa neno. Kanuni hii huwasilishwa kwa njia ifuatayo:

$$\left[+\text{Irabu}\right] > \emptyset \ / \ \left[+\text{Kons}\right] \ __\#$$

### b) Udondoshaji wa Silabi

Uchunguzi wetu pia umeonyesha kuwa udondoshaji huweza kuathiri silabi katika mchakato wa kiutohozi. Imebainika kuwa, udondoshaji wa silabi aghalabu huathiri silabi zilizomo ndani ya neno. Maneno yafuatayo yanadhihirisha hali hii:

| Kiswahili | Kijaluo |
|---|---|
| a. ba**ha**ʃa | basa |
| b. mka**ha**wa | magawa |
| c. sa**ha**ni | san |
| d. ru**hu**sa | rusa |

Katika maneno haya, silabi za Kijaluo zilizonukuliwa kwa herufi nzito ndizo hutoweka utohozi unapofanyika. Kanuni ya udondoshaji huu ni kuwa silabi ya pili kutoka mwisho wa neno (ya Kiswahili) hudondoshwa iwapo inaundwa kutokana na kikwamizwa hafifu cha koromeo pamoja na irabu.

Kwingineko, ingawa udondoshaji wa silabi ya mwisho hautokei kwa wingi kwenye mchakato wa utohozi, kuna maneno machache yanayodhihirisha hali hii:

| Kiswahili | Kijaluo |
|---|---|
| a. ŋguru**wɛ** | aŋguro |

Katika neno hili, ni silabi ya mwisho $wɛ$ ndiyo iliyoathiriwa na mfanyiko wa udondoshaji. Kwa jumla udondoshaji katika utaratibu wa kutohoa leksimu za Kijaluo (kutokana na Kiswahili) huelenga kuibua muundo wa silabi unaopendelewa katika neno husika. Kwa mujibu wa uchanganuzi wetu, muundo ambao hutokea baada ya mfanyikio huu mara nyingi ni ule wa silabi funge.

Ingawa udondoshaji unakiuka kanuni ya mkabala wa mlingano chanzi (kanuni ya uaminifu ambao unasisitiza mfanano kati ya umbo la lugha changizi na ule wa lugha pokezi), mkabala huo huo pia unaruhusu udondoshaji wa vipashio ambavyo si vya kimsingi katika mfumo wa lugha pokezi. Kwa hivyo, vipashio vinavyodondoshwa ni vile visivyo na umuhimu wa kimsingi katika leksimu zinazohusika kwa mujibu wa fonolojia ya lugha ya Kijaluo.

### 3.3.1.2 Ubadili wa Silabi

Ubadili wa silabi *(syllable replacement)* ni mchakato unaohusu uingizaji wa silabi fulani katika nafasi ya silabi nyingine ambayo hutoweka kwenye utaratibu wa utohozi. Uchanganuzi umebainisha kuwa silabi ya mwanzo ndiyo huathiriwa na mchakato huu. Silabi za mwanzo katika nomino za Kiswahili huondolewa na nafasi zao huchukuliwa na silabi ya Kijaluo $ɔ$. Maneno yafuatayo yanadhihirisha hali hii:

| Kiswahili | Kijaluo |
|---|---|
| a. ʃɛmɛji | ɔmɛǰɔ |
| b. **m**kwaǰu | ɔkwaǰu |
| c. **m**ʧɛlɛ | ɔʧɛlɛ |
| d. **ki**ɲɔzi | ɔɲɔsi |

Katika maneno haya, silabi za Kiswahili zilizoandikwa kwa herufi zilizokolea hutoweka na nafasi zao kuchukuliwa na silabi ya Kijaluo $ɔ$. Huu ndio ubadili wa silabi. Kanuni ya ubadili wa silabi inasema kuwa silabi ya mwanzo katika neno hubadilika na kuwa irabu ya nyuma kati katika mazingira ya kutokea mwanzoni mwa neno na kufuatwa na silabi nyingine. Sheria hii inawasilishwa kwa namna ifuatayo:

$$\begin{bmatrix}+\text{Silabi}\end{bmatrix} > \begin{bmatrix}+\text{Irabu}\\+\text{Kati}\\+\text{Nyuma}\end{bmatrix} \Big/ \#__ \begin{bmatrix}+\text{Silabi}\end{bmatrix}$$

Hata hivyo, mageuko ya aina hii yanatokea katika baadhi ya nomino mkopo pekee tu bali si nomino zote za mkopo. Sababu ni kuwa, kuna miundo mingine ya silabi ambayo inaweza kujitokeza katika nafasi ya mwanzo kwenye maneno-mkopo. Miundo hiyo mingine ni kama vile muundo wa KI.

### 3.3.1.3 Uchopekaji

Uchopekaji ni uingizaji wa kipashio katika mazingira maalum ya kifonetiki. Njogu na wengine (2006) wanaeleza kuwa uchopekeji hutumika kudhibiti muundo asilia wa lugha. Muundo unaorejelewa hapa ni ule wa silabi za neno. Kwa mfano, katika Kiswahili, uchopekaji hutumika kwa wingi katika maneno mkopo ya Kiswahili kwa lengo la kuepuka silabi funge mwishoni mwa neno na pia kuibua muundo wa silabi unaopendelewa na lugha ya Kiswahili wa KI (Iribemwangi, 2010). Uchopekaji unaweza kuhusisha sauti za irabu au sauti za konsonanti. Uchopekaji wa irabu ni uingizaji wa sauti ya irabu katikati ya sauti za konsonanti zinazofuatana katika neno. Utaratibu huu hulenga kuvunja msururu wa sauti za konsonanti katika maneno yanayotoholewa.

Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa uchopekaji unaotokea katika harakati za kukopa maneno (kutokana na Kiswahili) unachukua sura mbili tofauti: uchopekeji-mwanzo na uchopekaji-kati. Uchopekaji-mwanzo wa silabi unahusu uingizaji wa silabi/fonimu katika nafasi ya mwanzo kwenye neno. Silabi $ɔ$ au $a$ hutiwa mwanzoni mwa neno linatoholewa. Maneno yafuatayo yanaonyesha hali hii:

| Kiswahili | Kijaluo |
|---|---|
| a. gunia | ɔgunia |
| b. piŋgu | ɔpiŋgɔ |
| c. ruŋgu | aruŋgu |
| d. ŋgumi | aŋgum |

Uchopekaji-mwanzo wa silabi unaongozwa na kanuni inayoeleza kwamba irabu hupachikwa mwanzoni mwa neno iwapo silabi ya mwanzo kwenye neno hilo ni ya KI. Tunaweza kuonyesha mfanyiko huu kupitia kanuni ifuatayo:

$$\emptyset \; > \; \begin{bmatrix} +\text{Silabi} \\ +\text{Irabu} \end{bmatrix} \Big/ \# __ \; \begin{bmatrix} +\text{Silabi} \end{bmatrix}$$

Mfanyiko huu pia hutokea katika baadhi ya maneno-mkopo pekee na si maneno yote ya mkopo. Sababu ni kuwa, kwa mujibu wa fonolojia ya Kijaluo, kunayo miundo mingine ya silabi ambayo inaweza kuchukua nafasi ya kwanza katika maneno-mkopo ya Kijaluo. Hata hivyo, mikhtadha ya kupachikwa/kutopachikwa kwa silabi hii haikubainika wazi kwenye uchanganuzi huu. Kwa hivyo, ni swala linalostahili kuchunguzwa zaidi.Vielelezo hivi vinaonyesha uchopekaji wa silabi $ɔ$ na $a$ mwanzoni mwa neno. Hata hivyo, uchanganuzi umebainisha kwamba silabi $ɔ$ ndiyo huchopekwa kwa wingi zaidi kwenye harakati za kutohoa maneno kutokana na Kiswahili. Silabi $a$ huchopekwa katika maneno machache tu.

Pia, ilitambuliwa kuwa uchopekaji-kati ambao unahusu uingizaji wa vipande-sauti katikati ya neno linalotoholewa pia hutokea kwenye utaratibu wa utohozi. Kwenye muktadha wa Kijaluo, irabu ndizo huingizwa mara nyingi. Uchopekaji wa aina hii hulenga kuunda silabi ya Kijaluo

yenye muundo wa KI kutokana na silabi za Kiswahili zinazoundwa kutokana na nazali moja pekee. Hali hii inaletwa na wazo kwamba nazali hazina sifa za usilabi katika lugha ya Kijaluo. Maneno yafuatayo yanadhihirisha hali hii:

| **Kiswahili** | **Kijaluo** |
| --- | --- |
| a. msumɛnɔ | **mu**smɛnɔ |
| b. mʃipi | **ma**sip |
| c. mswaki | **ma**swak |
| d. mzabibu | **mu**sabibu |

Katika maneno haya, uchopekaji wa irabu mbalimbali unaibua silabi za Kijaluo ambazo ni za KI kutokana na silabi ya Kiswahili ya nazali $m$. Sheria ya uchopekaji huu wa irabu ni kwamba irabu huchopekwa baada ya silabi ya mwanzo katika neno iwapo silabi hiyo ina muundo wa nazali moja pekee. Ufuatao ni uwasilishaji wa kanuni hii kwa kutumia sifa bainifu za kimatamshi:

$$\emptyset > \left[+\text{Irabu}\right] \Big/ \# \begin{bmatrix} +\text{Kons} \\ +\text{Nazali} \\ +\text{Ghuna} \\ +\text{Mdomo} \end{bmatrix} __ \left[+\text{Silabi}\right]$$

Masharti ya mkabala wa mlingano chanzi hayaruhusu uchopekaji katika mchakato wa kutohoa maneno. Hii inatokana na matakwa ya mkabala huu kwamba kuwe na mfanano baina ya vipashio vya lugha changizi na vile vya lugha pokezi. Hata hivyo, muundo wa lugha changizi unarojelewa na mkabala wa mlingano chanzi ni kama unavyofikiriwa na msemaji wa lugha pokezi (anayetohoa neno). Ili kupata muundo huu, vipengele vya kifonolojia vya lugha changizi

visiyopatikana katika lugha pokezi huweza kufanyiwa mabadiliko ambayo hatimaye huibua miundo inayokubalika katika mfumo wa lugha pokezi.

Mfano ni silabi za Kiswahili zenye miundo ya kifonolojia isiyokubaliwa katika fonolojia ya Kijaluo ambazo hugeuzwa ili kuzipatia miundo inayoruhusiwa na fonolojia ya Kijaluo. Hali hii inajitokeza katika mchakato wa kutohoa silabi za Kiswahili zinazoundwa kutokana na konsonanti moja ya nazali (muundo usiokubalika katika mfumo wa Kijaluo) ambazo huongezewa irabu ili kuleta muundo wenye kutambulika katika Kijaluo (muundo wa konsonanti-irabu). Hatimaye, muundo wa silabi ya Kiswahili ya nazali moja pekee (kama vile $m$) katika fikra za msemaji wa Kijaluo huweza kugeuka na kuwa nazali-irabu. Kulingana na mkabala wa mlingano chanzi, muundo wa lugha-changizi wa neno ni kama unavyofikiriwa na msemaji wa lugha pokezi. Muundo huu si lazima ufanane na muundo wa ndani wa neno linalokopwa. Hivyo basi, uchopekaji unamwezesha mkopaji kupata muundo lugha changizi unaozingatia fonolojia ya lugha pokezi.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumechanganua michakato ya utohozi wa kifonolojia wa leksimu za Kiswahili zinazoingingia katika lugha ya Kiswahili. Tumeona kuwa kuna mfanano kifonolojia baina ya vipande sauti vya lugha changizi na vile vya lugha pokezi kama inavyopendekezwa na mkabala wa mlingano chanzi; ingawa kuna maneno machache yanayokiuka hali hii kwa sababu mahususi. Hali hii inaonyesha kuwa mkabala wa mlingano chanzi ni nadharia inayoweza kutumiwa kueleza michakato ya kifonolojia inayohusishwa na utohozi wa maneno kutoka Kiswahili kuingia Kijaluo.

# SURA YA NNE

# UTOHOZI WA KIMOFOLOJIA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii itafafanua jinsi ambavyo leksimu za Kijaluo zinazotokana Kiswahili hutoholewa kimofolojia ndipo ziweze kuwasilisha maana zinazokubaliwa kwenye mfumo wa Kijaluo. Ili mikakati ya utohozi wa kimofolojia iweze kueleweka kikamilifu, tutaanza kwa kufafanua kimukhtasari vipengele vya mofolojia ya lugha tunazoshughulikia; yaani Kiswahili na Kijaluo. Maelezo haya yatadhihirisha tofauti/mifanano iliyopo baina ya mifumo ya kimofolojia ya lugha hizi mbili. Baada ya hapo, tutaonyesha mifumo ya viambishi vinavoambatishwa kwenye mizizi/mashina ya nomino-mkopo kwa mujibu wa kanuni za mofolojia ya Kijaluo.

Kuna tofauti za bainifu za kimofolojia kati ya lugha ya Kijaluo na lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, nomino za Kiswahili huwekwa makundi yanayotegemea viambishi awali katika nomino zenyewe; makundi haya ndiyo huitwa ngeli (kama ilivyobainishwa katika sehemu ya 2.3.2). Hali hii tofauti na Kijaluo ambayo nomino zake haziingizwi kwenye makundi yoyote. Badala yake, nomino za Kijaluo huwa na mfumo wa viambishi awali ambavyo hutumiwa kusimamia dhana mbalimbali.

## 4.2 Mikakati ya Utohozi wa Kimofolojia

Kiini cha sehemu hii ni kutathmini namna ambavyo maneno-mkopo huingizwa kwenye mfumo wa kimofolojia wa lugha ya Kijaluo. Kama anavyosema Smeaton (1973:83), maneno mkopo hupitia mageuzi ya kimofolojia ili yaweze kuwiana na mfumo wa lugha pokezi. Hivyo basi, leksimu hupitia mifanyiko mbalimbali inayoziwezesha kutumika kwa njia iliyo sawa na leksimu zingine za Kijaluo. Utaratibu huo ndio unaorejelewa kama utohozi wa kimofolojia.

Booij (2005) anatambua aina mbili za kategoria za kileksimu: kategoria wazi na kategoria funge. Kategoria wazi za kileksimu ni zile zinazoweza kupanuliwa kwa njia za uundaji-maneno. Kategoria hizo ni pamoja na nomino, vivumishi na vitenzi. Kwa upande mwingine, kategoria funge ni zile zisizoweza kupanuliwa kwa kutumia michakato ya uundaji-maneno. Hapa, kuna kategoria kama vile vibainishi, viunganishi, viwakilishi na vihusishi. Kwa vile utafiti huu unajikita katika utohozi wa nomino, tutadhihirisha jinsi ambavyo nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili huchukua viambishi anuwai vinavyofanikisha upanuzi wa leksimu katika kategoria hii ya maneno huku ikizingatiwa kuwa kategoria ya nomino ni wazi.

Kuna michakato mbalimbali ya kimofolojia ambayo inahusishwa na utohozi wa leksimu mkopo. Hata hivyo, ule unaotumika kwa wingi kwenye utohozi wa nomino za Kiswahili zinazoingia katika Kijaluo ni uambishaji. Uambishaji ni mchakato wa kuongeza viambishi katika shina/mzizi wa neno (Mccarthy, 2002). Uambishaji huweza kutokea kwa njia tatu tofauti: mwanzoni mwa shina/mzizi wa neno (uambishaji awali), katikati ya shina/mzizi wa neno (uambishaji ndani) na mwishoni mwa shina/mzizi wa neno (uambishaji tamati).

Uchunguzi wetu umedhihirisha kuwa Kijaluo hutumia uambishaji tamati kwa wingi zaidi katika kutohoa nomino za Kiswahili zinazoingia kwenye mfumo wa Kijaluo. Hii inamaana kuwa, mofimu mbalimbali huambatishwa mwishoni mwa mizizi/shina la nomino.Yaani, viambishi tamati hujitokeza kwa wingi katika nomino zilizokopwa kutokana na Kiswahili. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambacho hutumia kwa wingi zaidi mfumo wa viambishi awali katika nomino zake. Dhana zinazowasilishwa na viambishi hivi ni pamoja na idadi na hali ya umilikaji.

### 4.2.1 Viambishi vya Idadi katika Nomino Mkopo

Nomino za Kijaluo huchukua viambishi tamati ambavyo vinawakilisha mofimu tofautitofauti. Kwa mfano, mofimu ya wingi kila mara huwakilishwa na kiambishi tamati. Uchunguzi wetu

umeonyesha kuwa nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili huwa na mfumo wa viambishi ambao unafanana na ule wa nomino asilia za Kijaluo. Okombo (1982) anasema kuwa mofimu za wingi katika nomino za Kijaluo huwakilishwa na viambishi tamati {i}, {e} au {ni}.Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa nomino zilizokopwa huchukua mifumo hiyo hiyo ya viambishi. Vifuatavyo ni viambishi tamati vinavyowakilisha mofimu ya wingi katika nomino za mkopo: {ɛ}, {ndɛ}, {tʃɛ} na {ni}. Viambishi hivi vinajitokeza kwa namna zifuatazo katika nomino-mkopo:

**(a) Nomino zinazochukua kiambishi tamati {ɛ}**

Katika nomino hizi, nafasi ya irabu ya mwisho huchukuliwa na mofimu {ɛ} katika wingi. Hii inaonekana katika maneno yafuatayo:

| **Umoja (Kijaluo)** | **Wingi (Kijaluo)** | **Maana (Kiswahili)** |
|---|---|---|
| a. basa | bɛsɛ | bahasa |
| b. barasa | barɛsɛ | baraza |
| c. firimbi | firimbɛ | firimbi |
| d. ɔɲɔsi | ɔɲɔsɛ | kinyozi |

Hali kadhalika, konsonanti ya mwisho katika mzizi/shina huweza kubadilika na kuwa ghuna iwapo ilikuwa sighuna au kuwa sighuna iwapo ilikuwa ni ghuna. Maneno yafuatayo yanadhihirisha hali hii:

| **Umoja** | **Wingi** | **Maelezo (Umoja/Wingi)** |
|---|---|---|
| a. kabu**t** | kabu**d**ɛ | kaputi/kaputi |
| b. ti**g**a | ti**k**ɛ | twiga/twiga |
| c. kita**b**u | kitɛ**p**ɛ | kitabu/vitabu |
| d. ɔsi**g**ɔ | ɔsi**k**ɛ | mzigo/mizigo |

**(b) Nomino zinazochukua kiambishi {ʧɛ}**

Nomino hizi huchukua kiambishi {ʧɛ} ambacho huambatishwa kwenye mzizi kama kiambishi tamati; hii ni baada ya kudondoshwa kwa konsonanti ya mwisho kwenye shina/mzizi wa nomino pamoja na irabu ya mwisho katika nomino hiyo. Maneno yafuatayo yanaonyesha hali hii:

| Umoja | Wingi | Maana (Umoja/Wingi) |
|---|---|---|
| a. mapɛ**ra** | mapɛ**ʧɛ** | pera/mapera |
| b. matafa**re** | matafa**ʧɛ** | tofali/matofali |
| c. ɔkwa**ǰu** | ɔkwa**ʧɛ** | mkaju/mikwaju |
| d. saru**ru** | saru**ʧɛ** | sururu/sururu |

**(c) Nomino zinazochukua kiambishi tamati {ndɛ}**

Katika nomino hizi, konsonanti ya mwisho kwenye mzizi huondolewa na nafasi yake kuchukuliwa na kiambishi tamati {ndɛ}.

| Umoja | Wingi | Maana (Umoja/Wingi) |
|---|---|---|
| a. mɛ**li** | mɛ**ndɛ** | meli/meli |
| b. ɔchɛ**le** | ɔʧɛ**ndɛ** | mchele/michele |
| c. sirka**l** | sirka**ndɛ** | serikali/serikali |
| d. ɔki**l** | ɔki**ndɛ** | wakili/mawakili |

Mifano hii inaonyesha kuwa nomino zinazofuata mkondo huu ni zile ambazo mashina/mizizi yao inakamilika kwa konsonanti /l/.

**(d) Nomino zinazochukua kiambishi tamati {ni}**

Nomino hizi hupata wingi kwa kuambatishiwa kiambishi tamati {ni} kwenye mizizi/mashina yao baada ya kuondolewa kwa irabu zao za mwisho (iwapo irabu hiyo ipo). Vielelezo vifuatavyo vinaonyesha hali hii:

| Umoja | Wingi | Maana (Umoja/Wingi) |
|---|---|---|
| a. duka | duk**ni** | duka/maduka |
| b. kalɛnda | kalɛnd**ni** | kalenda/kalenda |
| c. ʧupa | ʧup**ni** | chupa/chupa |
| d. birika | birik**ni** | birika/birika |

Vielelezo hivi vinaonyesha kuwa leksimu za Kijaluo zilizotoholewa kutokana na Kiswahili zinachukua mifumo ya viambishi inayofanana na leksimu asilia za Kijaluo. Kwa mfano, imebainika kuwa nomino-mkopo huchukua viambishi tamati vinavyowakilisha mofimu za umoja/wingi sawa na nomino zingine za kawaida za Kijaluo (kama ilivyoonyeshwa katika sura ya pili). Viambishi vinavyochukuliwa na nomino mahususi hutegemea vipande-sauti vinavyounda nomino yenyewe. Kwa upande mwingine, imejitokeza kuwa hata ingawa nomino hizi hupokea mofimu mbalimbali kwa mujibu wa mofolojia ya Kijaluo, nomino zenyewe zimeweza kudumisha mfanano kwa kiasi kikubwa na lugha changizi (Kiswahili).

Pia, uchanganuzi umeonyesha kuwa mofu zote za Kiswahili za umoja/wingi hupoteza maana zao wakati neno linapotoholewa na kuingia kwenye mfumo wa kimofolojia wa Kijaluo. Zaidi ni kwamba, mofu hizo hubadilika na kuwa sehemu za mizizi ya maneno ya lugha pokezi. Uamilifu wa mofimu kama hizo huchukuliwa na vibadala vyao kwa mujibu wa kanuni za kimofolojia ya lugha pokezi (Kijaluo). Hali hii inatokana na dhana kwamba hakuna mfanano wowote wa

kimofolojia kati ya Kiswahili na Kijaluo kwani lugha hizi mbili zina mifumo inayotofautiana kabisa ya viambishi.

### 4.2.2 Viambishi vya Hali ya Umilikaji katika Nomino Mkopo

Katika sura ya pili (2.3.1.2), ilibainishwa kuwa hali ya umilikaji hurejelea maumbo tofautitofauti ya nomino ambayo huonyesha mahusiano ya kiumiliki kati ya nomino mbalimbali. Kwenye mukhtadha wa uchanganuzi huu wa maneno-mkopo, hali hizi zinaonyesha jinsi mahusiano ya kiumilikaji huwakilishwa katika nomino za Kijaluo ambazo zimekopwa kutokana na lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, tutabainisha namna ambavyo nomino hizi hupokea viambishi anuwai vya Kijaluo ambavyo vinaonyesha mahusiano ya kiumilikaji.

Katika lugha ya Kijaluo, nomino inayomilikiwa ndiyo inayofanyiwa mageuzi ya kimofolojia ambayo yanawezesha nomino yenyewe kuashiria mhusika mmiliki. Hii inamaanisha kwamba, mofimu yenye maana ya mhusika mmiliki huambatishwa katika mzizi wa nomino inayomilikiwa. Hii ni tofauti na Kiswahili ambayo huonyesha umilikaji kwa kutumia maneno maalum kama vile vihusishi. Katika Kijaluo, uchanganuzi unaonyesha kuwa nomino zote za mkopo (kutoka Kiswahili) zinaambatishiwa mofu za hali ya umilikaji kwenye mzizi wa nomino inayomilikiwa. Nomino kama hizo huchukua mofu mbalimbali ambazo zinadokeza umilikaji.

Kuna njia mbalimbali ambazo hutumiwa na maneno ya Kijaluo ili kuwasilisha hali ya umilikaji katika nomino (zilizokopwa kutoka lugha ya Kiswahili). Njia hizo ni kama zifuatazo:

**(a) Kwa kubadilisha toni ya matamshi ya nomino-mkopo**

Hapa, toni ya nomino husika hubadilishwa huku vipande-sauti huru vinavyojitokeza katika neno lenyewe vikibakia bila mageuzi yoyote. Mchakato huu hutokea hasa katika nomino za mkopo zisizokuwa na irabu ya mwisho katika miundo yao. Aghalabu nomino husika huwa na silabi za

mwisho ambazo ni funge. Dhana ya umilikaji katika nomino hizi hutambuliwa kupitia toni ya utamkaji wao. Toni hiyo aghalabu huwa ni ile ya kupanda. Maneno yafuatayo yanaonyesha hali hii:

| Nomino (Kiswahili) | Nomino (Kijaluo) | Hali ya Umilikaji | Maana |
|---|---|---|---|
| a. farasi | faras | faras | farasi wa |
| b. kamisi | kamis | kamis | kamisi ya |
| c. pasi | pas | pas | pasi ya |
| d. nazi | nas | nas | nazi ya |

**(b) Kwa kudondoa kiishio (irabu ya mwisho) katika nomino mkopo**

Mchakato huu hujitokeza tu katika nomino za mkopo ambazo zinaishia kwa silabi wazi. Nomino zifuatazo zinaonyesha hali hii:

| Nomino (Kiswahili) | Nomino (Kijaluo) | Hali ya Umilikaji | Maana |
|---|---|---|---|
| a. firimbi | firimbi | firimb | firimbi ya |
| b. gitaa | gita | git | gitaa ya |
| c. birika | birika | birik | birika ya |
| d. kiroboto | omboto | ombot | kiroboto wa |

Pia, kuna nomino nyingine ambazo hupata hali ya umilikaji kwa kubadilisha sifa ya konsonanti zao za mwisho. Hali hii huandamana na udondoshaji wa kiishio (irabu ya mwisho) katika neno lenyewe iwapo silabi yake ya mwisho ni wazi. Umbo ambalo ni tokeo la mageuzi hayo huwa na maana ya hali ya umilikaji. Vielelezo vifuatavyo vinadhihirisha hali hii:

| Nomino (Kiswahili) | Nomino (Kijaluo) | Hali ya Umilikaji | Maana |
|---|---|---|---|
| a. kaputi | kabu**t** | kabu**d** | kaputi ya |
| b. mshipi | masi**p** | masi**b** | mshipi wa |
| c. ndege | nde**ge** | nde**k** | ndege ya |
| d. kitabu | kita**bu** | kita**p** | kitabu cha |

**(c) Kwa kudondoa kiishio (silabi ya mwisho) cha nomino-mkopo na kutia mofu ya hali ya umilikaji {nd} au {ch}**

Hapa, kiishio hutoweka na nafasi yake huchukuliwa na mofimu ya hali ya umilikaji {nd} au {ch}. Kiishio kinachoondolewa kwa namna hii aghalabu huwa ni chenye muundo wa KI. Mifano ya nomino zinazopachikwa mofimu {nd} ni kama zifuatazo:

| Nomino (Kiswahili) | Nomino (Kijaluo) | Hali ya Umilikaji | Maana |
|---|---|---|---|
| a. meli | meli | mend | meli ya |
| b. mchele | ochele | ochend | mchele wa |
| c. msumeno | musmeno | musmend | musmeno ya |
| d. kalenda | kalenda | kalend | kalenda ya |

Kwingineko, iwapo nomino inashia kwa silabi-funge, basi kiambishi tamati kwenye silabi hiyo hudondoshwa na mofu ya hali ya umilikaji {ch} au {nd} huingizwa katika nafasi hiyo hiyo. Maneno yafuatayo yanaonyesha hali hii:

| Nomino (Kiswahili) | Nomino (Kijaluo) | Hali ya Umilikaji | Maana |
|---|---|---|---|
| a. majani | majan | majand | majani ya |
| b. sabuni | sabun | sabund | sabuni ya |
| c. wakili | okil | okind | wakili wa |
| d. safari | safar | safach | safari ya |

**(d) Kwa kuambatisha mofu ya hali umilikaji {mb} kama kiambishi tamati**

Pia kuna maneno machache ambayo hupokea kiambishi tamati {mb} kama mofimu ya hali ya umilikaji. Mara nyingi hali hii hutokea katika nomino ambazo zinaishia kwa nazali /m/. Katika hali hii, mofu {mb} huchukua nafasi ya nazali hiyo ya mwisho katika nomino. Ifuatayo ni mifano kamili:

| Nomino (Kiswahili) | Nomino (Kijaluo) | Hali ya Umilikaji | Maana |
|---|---|---|---|
| a. kalamu | kalam | kalamb | kalamu ya |
| b. sumu | sum | sumb | sumu ya |

## 4.3 Mifanyiko ya Utohozi wa Kimofolojia na Mkabala wa Mlingano Chanzi

Katika sura ya kwanza, ilibainishwa kuwa uchunguzi huu utatekelezwa katika msingi wa mkabala wa mlingano chanzi kama ulivyoasisiwa na Smith (2009). Ilisisitizwa kuwa mkabala huu unatawaliwa na mihimili miwili mikuu. Kwanza, vipande-sauti vyote vilivyomo katika neno changizi sharti vijitokeze katika neno pokezi. Pili, vipande sauti vyote vya lugha pokezi sharti viwepo katika lugha changizi.

Uchanganuzi wa mabadiliko ya kimofolojia kwenye leksimu za mkopo umeonyesha kuwa mabadiliko hayo yanatokea katika mipaka ya kanuni za mkabala wa mlingano chanzi. Hii ina

maana ya kwamba, licha ya leksimu za mkopo kufanyiwa mageuzi ya kimofolojia, leksimu hizo bado zinadumisha mfanano na lugha changizi.

Data zimeonyesha kuwa leksimu za Kijaluo zenye asili katika Kiswahili zinalingana pakubwa na leksimu changizi (za Kiswahili) hata baada ya leksimu hizo kupitia mabadiliko ya kimofolojia. Ingawa mabadiliko haya huandamana na nyongeza au kuondolewa kwa vipande sauti fulani vinavyojenga maneno-mkopo, maneno haya yanadumisha vipande-sauti vingi ambavyo vinatokana na lugha ya Kiswahili. Vielelezo vifuatavyo vinadhihirisha hali hii:

| **Neno Changizi** | **Neno Pokezi (Kijaluo)** | |
|---|---|---|
| **(Kiswahili)** | **Umoja** | **Wingi** |
| a. bɛndɛra | *bandɛra* | *bande*ʧe |
| b. dɛbɛ | *dɛbɛ* | *dɛ*pɛ |
| c. msumɛnɔ | *musmɛnɔ* | *musmɛn*dɛ |
| d. duka | *duka* | *duk*ni |

Vipande-sauti vyote vilivyonukuliwa kwa herufi za mlazo ni vile ambavyo vimedumishwa hata baada ya uambishaji kutokea. Vielelezo hivi vinaonyesha kuwa vipande-sauti vingi vinayopatikana katika leksimu za Kijaluo (zilizotoholewa kutokana na Kiswahili) vinabakia jinsi vilivyo hata kama leksimu zenyewe zinapopitia michakato ya kimofolojia (kama vile uambishaji). Yaani, michakato ya utohozi wa kimofolojia inajaribu kadri inavyowezekana kudumisha mfanano kati ya leksimu ya Kijaluo na ile ya lugha changizi (Kiswahili). Kwingineko ambako kuna mabadiliko katika vipande sauti mahususi katika leksimu ya lugha pokezi, matokeo ya mabadiliko kama hayo huwa ni sauti inayokaribiana kifonetiki na kipande-sauti cha neno changizi. Hali hii inawiana na kanuni ya mkabala wa mlingano chanzi ya kuwepo kwa mlingano katika vipande-sauti vya lugha-changizi na vile vya lugha-pokezi.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia michakato ya kimofolojia inayohusishwa na utohoji wa nomino za Kiswahili zinazoingia kwenye mfumo wa lugha ya Kijaluo. Imebainika kuwa, uambishaji ndio mchakato wa kimofolojia unaotumika kwa wingi zaidi kwenye utohozi wa aina hii. Hali kadhalika, mofimu nyingi zinazoambatishwa katika mizizi/mashina ya nomino hizi ni viambishi tamati. Pamoja na hayo, imeonyeshwa kuwa mifanyiko yote ya utohozi wa kimofolojia inahakikisha kuwa kuna ulinganifu wa kiwango fulani baina ya vipande-sauti vya lugha changizi (Kiswahili) na vile vya lugha pokezi (Kijaluo). Hali hii inawiana na masharti ya mkabala wa mlingano chanzi ambao ndio msingi wa uchanganuzi huu.

# SURA YA TANO

# MUKHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii itaangazia vipengele vitakavyohitimisha utafiti huu ambao kiini chake kilikuwa ni utohozi wa kifonolojia na kimofolojia wa maneno-mkopo; maneno yaliyochunguzwa yakiwa ni nomino za Kijaluo zilizotoholewa kutoka Kiswahili. Vipengele hivyo ni: mukhtasari wa matokeo, hitimisho pamoja na mapendekezo juu ya uchunguzi zaidi.

## 5.2 Mukhtasari wa Matokeo

Uchunguzi huu ulidhamiria kuchanganua namna ambavyo maneno ya Kiswahili hutoholewa kabla ya kuingizwa katika mfumo wa Kijaluo. Viwango vya utohozi ambavyo vililengwa ni viwili: kiwango cha fonolojia na cha mofolojia. Hivyo basi, utafiti ulijikita katika mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia ambayo maneno ya Kiswahili hupitia ili yaweza kutambuliwa kama msamiati wa Kijaluo. Taratibu hizi zote ziliongozwa na mkabala wa mlingano chanzi.

Mijadala kuhusu matokeo ya utafiti iligawanywa katika sehemu mbili kuu: utohozi wa kifonolojia ambao ulishughulikiwa kwenye sura ya tatu na kisha utohozi wa kimofolojia ambao umejadiliwa katika sura ya nne. Kuhusu utohozi wa kifonolojia, ilibainika kuwa utohozi wa aina hii hutokea katika kiwango cha fonimu na kiwango cha silabi. Kwenye utohozi wa fonimu, ilijitokeza kuwa kuna mifanyiko miwili mikuu ya kiutohozi: udumishaji wa sauti na ubadilishaji wa sauti. Udumishaji wa sauti ulihusu uingizaji wa sauti za irabu/konsonanti za Kiswahili moja kwa moja katika mfumo wa Kijaluo bila kuzifanyia mageuzi yoyote. Kwingineko, ubadilishaji wa sauti ulihusu ugeuzaji wa irabu/konsonanti za Kiswahili kabla ya kuziingiza katika mfumo wa Kijaluo.

Kuhusu utohozi wa silabi, michakato iliyohusika ni uchopekaji, udondoshaji na ubadili wa silabi. Uchopekaji ulihusu uingizaji wa kipashio katikati ya neno ili kuvunja msururu fulani wa sauti. Msururu huo unaweza kuwa wa sauti za konsonanti au wa irabu. Katika muktadha wa Kijaluo, uchopekaji ulilenga kuibua muundo wa silabi za KI hasa kutokana na silabi za Kiswahili zilizoundwa na sauti ya nazali moja pekee. Udondoshaji nao ulihusu kutoweka kwa sauti fulani katika neno katika mazingira maalum ya kifonolojia. Katika muktadha wa Kijaluo, lengo likiwa ni kupata silabi zenye muundo wa silabi funge. Hii inatokana na dhana kwamba, lugha ya Kijaluo huruhusu mfumo wa silabi funge, hali ambayo haipatikani katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingi za Kibantu. Hali kadhalika, tulishuhudia ubadili wa silabi ambapo silabi za mwanzo za maneno ya Kiswahili huondolewa na nafasi zao kuchukuliwa na silabi nyingine ya Kijaluo.

Katika sura ya nne, mjadala wetu ulijikita katika utohozi wa kimofolojia ambapo ilibainika kwamba uambishaji unatumika kwa wingi kama mchakato wa kiutohozi wa kimofolojia. Tulifasili uambishaji kama mchakato wa kupachika viambishi anuwai kwenye mzizi/shina la neno.Viambishi vyenyewe huweza kuwa viambishi-awali, viambishi-kati au viambishi-tamati. Hata hivyo, iligunduliwa kuwa viambishi tamati ndivyo hutumiwa mara nyingi zaidi utohozi wa kimofolojia unapofanyika. Aghalabu viambishi hivi huwa ni vile vinavyosimamia mofimu ya wingi na hali ya umilikaji. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambacho huwasilisha wingi wa nomino zake kupitia mofimu zinazowakilishwa na viambishi-awali. Katika harakati hizi, viambishi vya Kiswahili vya kusimamia idadi hupoteza maana zao na kujumuishwa kama sehemu za mizizi ya nomino (wakati wa utohozi).

Hatimaye, ilidhihirika kuwa ingawa maneno ya Kiswahili hupokea mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia katika mchakato wa kiutohozi kabla ya kutambuliwa kama neno kamili la Kijaluo, hatimaye kuna mfanano kati ya umbo la neno la lugha pokezi (Kijaluo) na lile la lugha changizi

(Kiswahili) lililokopwa. Kuwepo kwa mfanano wa aina hii huelezeka kwenye mkabala wa mlingano chanzi ambao uliasisiwa na Smith (1999); mtazamo ambao ndio nadharia inayoelekeza utafiti huu.

Ilidokezwa kuwa, kanuni ya uaminifu ndiyo mhimili wa mkabala huu wa mlingano chanzi. Mfanano unaorejelewa kwenye mkabala huu hutokea katika vipande-sauti vinavyounda neno-pokezi na vile vya neno-changizi. Kwa jumla, mtazamo huu wa mlingano chanzi uliweza kufafanua kikamilifu mchakato mzima wa utohozi wa kifonolojia na kimofolojia.

## 5.3 Tathmini ya Nadharia Tete na Matokeo ya Utafiti

Kama ilivyobainishwa katika sura ya kwanza (1.4), utafiti huu uliekezwa na nadharia tete tatu kuu.Tathmini ya nadharia tete hizi dhidi ya matokeo ya utafiti zinaonyesha kuwa nadharia tete zote za uchunguzi huu zimethibitishwa. Kwa kuanzia, nadharia tete ya kwanza iliyodai kuwa maneno-mkopo ya Kijaluo (kutoka Kiswahili) hupitia michakato mbalimbali ya kifonolojia kabla ya kutambuliwa kama msamiati wa Kijaluo. Nadharia tete hii ilithibitishwa kwenye sura ya tatu ambapo ilibainika kuwa maneno ya Kiswahili hupitia mifanyiko anuwai kwenye harakati za utohozi. Miongoni mwa michakato hiyo ni pamoja na udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa sifa za fonimu. Michakato hii hulenga kuibua muundo wa silabi pendwa katika lugha ya Kijaluo (silabi yenye muundo wa konsonanti-irabu au konsonanti-irabu-konsonanti).

Nadharia tete ya pili nayo ilidokeza kuwa maneno mkopo kutoka Kiswahili yanapitia michakato mbalimbali ya kimofolojia kabla ya kuingizwa kwenye mfumo wa Kijaluo. Nadharia tete hii ilithibitishwa kwenye mjadala wa sura ya nne ambapo ilibainika kuwa mchakato wa uambishaji ndio hutumiwa zaidi katika utohozi wa kimofolojia. Hapa, tulionyesha kuwa viambishi-tamati ndivyo hutumiwa mara nyingi kwenye utohozi wa kimofolojia. Kwa mfano, ilidhihirika kuwa mofimu ya idadi katika nomino za Kijaluo mara kwa mara huwasilishwa

kupitia viambishi-tamati. Viambishi hivi hutegemea miundo ya mashina/mizizi ya nomino husika.

Kwingineko, haipothesia ya tatu ilisema kuwa kuna ulinganifu wa kifonolojia na kimofolojia baina ya vipashio vya lugha changizi na vile vya lugha pokezi. Nadharia tete hii ilithibishwa kwenye sura za tatu na nne tulipokuwa tukijadili utohozi wa kifonolojia na kimofolojia mtawalia. Kuhusu mlingano wa kifonolojia, ilibainika kwamba vipande sauti vingi vya lugha-changizi (Kiswahili) hudumishwa katika lugha-pokezi (Kijaluo) utohozi unapotokea. Hata kama sauti ya lugha-changizi imebadilika kwenye harakati za kiutohozi, sauti ambayo ni tokeo (katika lugha-pokezi) aghalabu huwa na mahusiano ya karibu ya kifonetiki na ile ya lugha changizi. Kwenye kitengo cha kimofolojia, ilibainika kuwa uambishaji ni mchakato unaotokea kwa wingi katika utohozi wa nomino za lugha zote mbili zilizoshughulikiwa: Kiswahili na Kijaluo. Hata hivyo, tulibaini kuwa Kijaluo hupendelea mfumo wa viambishi-tamati kama mofimu ya idadi nayo Kiswahili inatumia viambishi-awali kuwasilisha mofimu ya idadi.

## 5.4 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya uchunguzi wetu, imebainika kuwa mkabala wa mlingano chanzi unaweza kutumiwa kufafanua mchakato wa kiutohozi katika katika lugha mahususi. Katika muktadha wa utafiti huu, hali zinazodhihirika maneno yanapotoholewa kutoka lugha ya Kiswahili kuelekea lugha ya Kijaluo zinaweza kueleweka vyema kwenye mkabala wa mlingano chanzi. Kwa mfano, hali ya mfanano uliopo baina ya vipashio vya lugha-changizi na vile vya lugha-pokezi hueleweka kwenye misingi ya kanuni za mkabala wa mlingano chanzi. Kipengee ambacho kinasisitizwa na kanuni zenyewe ni kuwepo kwa ulinganifu katika maumbo ya vipande-sauti vya lugha-changizi na vile vya lugha-pokezi. Hii inamaanisha kuwa udondoshaji na uchopekaji haupendelewi kwenye mchakato mzima wa kiutohozi.

Hata hivyo, maumbo yanayorejelewa na yanayotarajiwa kulingana katika lugha mbili zilizohusika ni umbo fikirika la lugha-changizi na umbo-tamkwa la lugha-pokezi. Ni katika muktadha huu ambapo tunapata michakato mbalimbali ya kiutohozi kwenye viwango vya kifonolojia na kimofolojia; masuala ambayo ndiyo yamekuwa kiini cha utafiti huu.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Uchunguzi wetu ulijikita kwenye utohozi wa maneno-mkopo yanayoingia katika lugha ya Kijaluo kutoka Kiswahili. Katika mchakato huo wote, viwango viwili vya kiisimu vilizingatiwa: fonolojia na mofolojia. Hata hivyo, utohozi huweza kutokea hata katika viwango vingine vya kiisimu kama vile sintaksia na pragmatiki. Hivyo, ni pendekezo letu kuwa utafiti ufanywe katika viwango hivi ili kubaini michakato ya kiisimu inayohusishwa na utohozi kwenye ngazi hizo.

Pia, utafiti huu ulishughulikia vipande-sauti huru, yaani konsonanti na irabu pekee.Hata hivyo, utohozi pia hutokea katika kiwango cha fonolojia arudhi. Hivyo basi, ni maoni yetu kuwa uchunguzi uweze kufanywa kuhusu utohozi kiarudhi katika muktadha wa maneno ya Kijaluo yaliyotoholewa kutoka Kiswahili. Swala hili ni muhimu kwani lugha ya Kijaluo ina vipengele vingi vya kifonolojia arudhi kama ilivyo kwenye lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, ni muhimu kuchanganua namna ambavyo vipengele vya fonolojia arudhi vya Kiswahili hukabiliwa wakati neno la Kiswahili linapotoholewa na kuingizwa katika mfumo wa Kijaluo.

Hali kadhalika, ni pendekezo letu kuwa utafiti kuhusu utohozi wa maneno ya kategoria zingine uweze kufanywa. Sababu ni kwamba, utafiti huu ulijikita katika nomino pekee licha ya kwamba kuna maneno ya Kijaluo (kama vile vitenzi) ambayo yametoholewa kutoka Kiswahili. Hivyo, kuna umuhimu katika kuchanganua mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia inayohushwa na utohozi wa maneno kama hayo.

# MAREJELEO


Adhiambo, J. H. (1981). Dholuo Phonology: A Study of the Major Vowel Processes. Unpublished master's dissertation; University of Nairobi, Nairobi.

Anttila, R. (1972). *Introduction to Historical and Comparative Linguistics.* London: Macmillan Publishers.

Booij, G. (2005). *The Grammar of Words.* New York: Oxford University Press.

Campbell, G. L. (1991). *Compendium of the World's Languages*. Vol.II London: Routledge.

Cohen, D. W. (1974). The River Lake Nilotes from the Fifteen to the Nineteenth Century. In B.A Ogot, J. A. Kieran, (Ed): *Zamani: A Survey of East African History*. Nairobi: Longman Kenya.

Crystal, D. (1976). *Prosodic Systems and Intonation in English.* Cambridge: Cambridge University Press.

Grimes, E. (1996). *Ethnologue: Languages of the World*. Dallas: SIL. 13th Ed.

Iribemwangi, P. I. & Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.

Iribemwangi, P. I. (2010). *The Structure of Kiswahili: Sounds, Sound Changes and Words.* Saarbrucken: VDM Verlag.

Iribemwangi, P. I. (2013). Cultural Transfer from Europe and Asia to Africa: Evidence from Borrowed Lexicon Adapted into Kiswahili .In *International Journal of Education and Research*. Vol. 1 No. 8 Pg. 1-14.

Karuru, I. (2012). "Pholonogical and Morphological Adaptation of Gi – Gichugu: An Application of Source – similarity Model". Unpublished master's project, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Kimani, R. G. (2005). "A Phonotactic Adaptation of Masaai Loanwords into Gikuyu Language". Unpublished master's thesis, University of Nairobi, Nairobi.

Lehman, W. P. (1975). *Historical Linguistics: An Introduction.* New York: HoH Rinehart and Winston.

Mbonankira, G. (2004). "The Accommodation of Kiswahili and English Words into Kinyarwanda". Unpublished Master's thesis, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

McCarthy, A. C. (2002). *An Introduction to English Morphology: Words and their Structure.* Edinburg: Edinburg University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mugenda, A. G. (2008). *Social Science Research: Theory and Principles.* Nairobi: Acts Press.

Mwaliwa, H. C. (2014). "An analysis of the syllable structure of standard Kiswahili loanwords from modern standard Arabic". Unpublished Doctoral thesis, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Mwita, L. C. (2009). Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint Based Analysis. In *The Journal of Pan African Studies;* Vol. 2*, No. 2, 46-61.*

Ngala, J. A. (1994). A Contrastive Analysis of the English (RP) and Dholuo Syllable Structures. M. A. Dissertation, Moi University, Eldoret.

Njogu et.al, (2006). *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: JKF.

Ochieng', W. (1985). *History of Kenya.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Oduor, J. A. N. (2002). "A Study of Syllable Weight and its Effects in Dholuo Phonology". Unpublished doctoral thesis, University of Nairobi.

Okombo, D. (1982). *Dholuo Morphophonemics in a Generative Framework.* Berline Beiner.

Oluoch, Y. J. (2014). "Loanword Adaption in Boro – Ukwala Dialect of Dholuo: A Case of Borrowing from Lumarachi, Lunyala and Kiswahili". Unpublished Master's project, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Owino, D. (2003). "Phonological Nativization of Dholuo Loanwords". Unpublished Master's thesis, University of Pretoria, Pretoria, South Africa.

Polome, E. (1967). *Swahili Handbook.* Washington, D.C.: Centre for Applied Linguistics.

Smith, J. L. (2006b). Loan Phonology is not all Perception: Evidence from Japanese loan doublets. In T. J. Vance & K. A. Jones (Eds.) *Japanese /Korean linguistics*, *Volume 14*, 63-74. Stanford: CSLI.

Stafford R. L. (1967). *An Elementary Dholuo Grammar with Vocabularies*. Nairobi: OUP.

Suleh, E. A. (2013). "A Morphosyntactic Analysis of Ambiguity of Mood in Dholuo: The Minimalist Programme Approach (1995)".Unpublished PhD Thesis, University of South Africa.

Tucker, A. N. (1994). *A Grammar of Kenya Luo (Dholuo).* Koln: Rudiger, Koppee, Verlag. Unpublished master's thesis, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

## KIAMBATISHO

## MANENO-MKOPO YA KIJALUO KUTOKA KISWAHILI

Ifuatayo ni orodha ya maneno ya Kijaluo (yaliyokusanywa) yaliyotoholewa kutokana na lugha ya Kiswahili. Maneno haya yamepangwa kialfabeti na kunukuliwa kiothografia na kifonetiki katika lugha ya Kijaluo na Kiswahili mtawalia.

| | KISWAHILI | | KIJALUO | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | UNUKUZI KIOTHOGRA-FIA | UNUKUZI KIFONETI-KI | UNUKUZI KIOTHOGRA-FIA | UNUKUZI KIFONETIKI | |
| | | | | UMOJA | WINGI |
| 1. | bahasha | bahaʃa | basa | basa | bɛsɛ |
| 2. | bakuli | bakuli | bakul | bakul | bakundɛ |
| 3. | baraza | baraza | barasa | barasa | barasɛ |
| 4. | barua | barua | baruwa | baruwa | barupɛ |
| 5. | bata | bata | mbata | mbata | mbɛtɛ |
| 6. | bɛndɛra | bɛndɛra | bandera | bandɛra | bandɛʧɛ |
| 7. | birika | birika | birika/brika | birika | birikni/birikɛ |
| 8. | buibui (mdudu) | buibui | mbui | mbui | mbuʧɛ |
| 9. | ʧampali | ʧampali | champat | ʧampat/ɔpatɔ | ʧampɛtɛ/ɔpɛtni |
| 10. | ʧupa | ʧupa | chupa | ʧupa | ʧupni |
| 11. | dɛbɛ | dɛbɛ | debe | dɛbɛ | dɛpɛ |
| 12. | duka | duka | duka | duka | dukni |
| 13. | farasi | farasi | faras | faras | farɛsɛ |
| 14. | filimbi | filimbi | firimbi | firimbi | firimbɛ |
| 15. | ghasia (takataka) | ɣasia | gasia | gasia | gasɛʧɛ |
| 16. | gitaa | gitaa | gita | gita | gitni |
| 17. | godoro | gɔdɔrɔ | godhro | gɔðrɔ | gɔðrɔʧɛ |
| 18. | gunia | gunia | ogunia | ɔgunia | ɔgundɛ |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 19. | jikoni | ǰikɔni | jikon/ jokon | Ɉikɔn/Ɉɔkɔn | Ɉikɔndɛ/Ɉɔkɔndɛ |
| 20. | jumamosi | ǰumamɔsi | jumamos | Ɉumamɔs | Ɉumamɔsɛ |
| 21. | jumapili | ǰumapili | jumapil | Ɉumapil | Ɉumapindɛ |
| 22. | kalamu | kalamu | kalam | kalam | kalɛmbɛ |
| 23. | kalɛnda | kalɛnda | kalenda | kalɛnda | kalɛndɛ/ kalɛndni |
| 24. | kamisi | kamisi | kamis | kamis | kamisɛ |
| 25. | kaputi | kaputi | kabut | kabut | kabudɛ |
| 26. | karatasi | karatasi | kalatas/otas | kalatas/ ɔtas | kalatɛsɛ/ ɔtɛsɛ |
| 27. | kikapu | kikapu | okapu | ɔkapu | ɔkɛpɛ |
| 28. | kinyozi | kiɲɔzi | kinyosi/onyosi | kiɲɔsi/ɔɲɔsi | kiɲɔsɛ/ ɔɲɔsɛ |
| 29. | kiroboto | kirɔbɔtɔ | omboto | ɔmbɔtɔ | ɔmbɔtɛ |
| 30. | kitabu | kitabu | kitabu | kitabu | kitɛpɛ |
| 31. | kitunguu | kituŋguu | kitungu | kituŋgu/ɔtuŋgu | kituŋgɛ/ ɔtuŋgɛ |
| 32. | kura | kura | kura | kura | kuʧɛ |
| 33. | mafuta | mafuta | mauta/ mafuta | mauta/ mafuta | mautɛ/ mafutɛ |
| 34. | majani | maǰani | majan | maɈan | maɈɛndɛ |
| 35. | makasi | makasi | makas | makas | makasɛ |
| 36. | mananasi | mananasi | mananas | mananas | mananɛsɛ |
| 37. | mapɛra | mapɛra | mapera | mapɛra | mapɛʧɛ |
| 38. | matofali | matɔfali | matafare | matafarɛ | matafaʧɛ |
| 39. | mchele | mʧɛlɛ | ochele | ɔʧɛlɛ | ɔʧɛndɛ |
| 40. | meli | mɛli | meli | mɛli | mɛndɛ |
| 41. | mihogo | mihɔgɔ | mwogo/ omwogo | muɔgɔ/ ɔmwɔgɔ | muɔkɛ/ ɔmuɔkɛ |
| 42. | mkahawa | mkahawa | magawa | magawa | magɛpɛ |
| 43. | mkɛbɛ | mkɛbɛ | okebe | ɔkɛbɛ | ɔkɛpɛ |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 44. | mkongɛ | mkɔŋgɛ | makonga | makɔŋga | makɔŋgɛ |
| 45. | mkwaju | mkwaǰu | okwaju | ɔkwaɟu | ɔkwaʧɛ |
| 46. | mshipi | mʃipi | masip | masip | masibɛ |
| 47. | msumɛno | msumɛnɔ | musmeno | musmɛnɔ | musmɛndɛ |
| 48. | mswaki | mswaki | maswak | maswak | maswagɛ |
| 49. | mzabibu | mzabibu | musabibu | musabibu | musabipɛ |
| 50. | mzigo | mzigɔ | osigo/<br>misigo | ɔsigɔ/<br>misigɔ | ɔsikɛ/<br>misikɛ |
| 51. | mzungu | mzuŋgu | misungu | misuŋgu | misuŋgɛ |
| 52. | nazi | nazi | nas | nas | nɛsɛ |
| 53. | ndɛgɛ<br>(ya usafiri) | ndɛgɛ | ndege | ndɛgɛ | ndɛkɛ |
| 54. | ndimu | ndimu | ndim | ndim | ndimɛ |
| 55. | ngumi | ŋgumi | angum | aŋgum | aŋgumɛ |
| 56. | nguruwɛ | ŋguruwɛ | anguro | aŋgurɔ | aŋguʧɛ |
| 57. | njugu | ɲǰugu | njugu | ɲɟugu | nɟukɛ |
| 58. | nusu | nusu | nus | nus | nusɛ |
| 59. | pasi | pasi | pas | pas | pɛsɛ/pɛsni |
| 60. | pɛsa | pɛsa | pesa | pɛsa | pɛs |
| 61. | ʧumvi | ʧumvi | chumbi | ʧumbi | ʧumbɛ |
| 62. | pikipiki | pikipiki | apiko | apikɔ | apigɛ |
| 63. | pingu | piŋgu | opingo | ɔpiŋgɔ | ɔpiŋgɛ |
| 64. | rɛli | rɛli | reru | rɛru | rɛʧɛ |
| 65. | risasi | risasi | lisasi | lisasi | lisɛʧɛ |
| 66. | ruhusa | ruhusa | rusa | rusa | rusɛ |
| 67. | rungu | ruŋgu | arungu/rungu | aruŋgu/ruŋgu | aruŋgɛ/ruŋgɛ |
| 68. | sabuni | sabuni | sabun | sabun | sabundɛ |
| 69. | sadaka | sadaka | sadaka | sadaka | sadɛkɛ |
| 70. | safari | safari | safar | safar | safaʧɛ |
| 71. | sahani | sahani | san | san | sandɛ |
| 72. | sɛrikali | sɛrikali | sirikal/sirkal | sirikal/sirkal | sirkɛndɛ |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 73. | shɛmɛji | ʃɛmɛǰi | semeji | sɛmɛǰi/ɔmɛǰɔ | sɛmɛʧɛ/ɔmɛʧɛ |
| 74. | siasa | siasa | siasa | siasa | siaɛsɛ |
| 75. | sumu | sumu | sum | sum | sumbɛ |
| 76. | sururu | sururu | saruru | saruru | saruʧɛ |
| 77. | tangawizi | taŋgawizi | tangausi | taŋgausi | taŋgausɛ |
| 78. | tarɛhɛ | tarɛhɛ | tarik | tarik | tarigɛ |
| 79. | twiga | twiga | tiga | tiga | tikɛ |
| 80. | wakili | wakili | okil | ɔkil | ɔkindɛ |